# Nipashe

Jumamosi Agosti 8, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580305

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Serikali yaeleza ilivyovunja rekodi katika ukuaji uchumi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Membe: Nitakuwa Rais wa watu wote

• **Achukua** fomu Tume ya Uchaguzi, aahidi kampeni za kistaarabu, NCCR- Mageuzi yapata wagombea Tanzania, Zanzibar...*Endelea ukurasa 2*




Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage (kulia), akikabidhi kwa mgombea urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Benard Membe, mkoba wenye fomu za kuomba kuteuliwa na Tume hiyo, kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika ofisi za tume hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### UJENZI RELI YA SGR WAMKUNA MAJALIWA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alikagua ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) na kueleza kuridhishwa na kasi ya...

UKURASA WA 4

### TPSF YAJITOSA VITA UJANGILI

TAASISI ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), imesema serikali inatakiwa kushirikiana nayo katika mapambano dhidi ya ujangili badala ya...

## Ajali ya gari yaua wanafunzi watatu

UKURASA 3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store


## ... Mgombea mwingine atinga NEC pekupeku

UKURASA 2




MICHEZO AZAM BADO WANNE TU, SHIBOUB ATAJWA UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

## NCCR wapitisha wagombea urais

**Na Romana Mallya**

MKUTANO Mkuu wa Chama cha NCCR-Mageuzi, ulifanyika jana jijini Dar es Salaam, kupitisha wagombea wa chama hicho kwenye nafasi ya urais wa Tanzania Bara na Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia, alisema ni vizuri mtu akiwa madarakani aweke mfumo utakaosaidia taifa.

"Ndiyo maana chama chetu tunataka katika mfumo wa elimu kuongeza 'K' nyingine yenye maana ya kusikiliza," alisema.

Alisema chama chao kimejengwa na misingi mitatu na kuitaja baadhi kuwa ni katiba ambayo wameipigania zaidi ya miaka 29 na msingi mwingine ni uchumi unaoendana na elimu.

Mbatia alisema ni lazima kuzilinda ndimi ili kuiacha nchi kwenye amani.

"Unaweza kumtoa nyoka pangoni kwa kutumia ndimi, NCCR Mageuzi iwe kielelezo cha kutumia ndimi vizuri kwa maisha ya Watanzania miaka mitano ijayo kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Tutumie ndimi zetu siyo kwa kuogopa, la hasha, kwa kusema ukweli, nchi hii ni yetu sote," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Julius Nyerere, Joseph Butiku (82), alitaja mambo ya msingi aliyoshuhudia katika maisha yake yote, akisema:

"Msione vinaelea vimeundwa, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, mkutano unatafuta wagombea urais, mnaowatafuta siyo waasisi, ni wale wanaokubali kurithi, kurithishwa mema ya hao waliotangulia," alisema.

Butiku alisema kila akimwona Mbatia ndani yake ni mtu aliyetosheka, aliyelelewa, hivyo kazi yake ni kuwalea hao wote.

"Ninyi hamzungumzi rushwa, nani anatoa, nani anapokea? Kama katika chama hiki haipo, ninawapongeza, ninaomba isiwapo. Mimi ni mwanachama wa CCM, ipo, sisemi kuwachongea, ninasema kweli.

"Watoa rushwa ni Watanzania, wale wanaCCM ni wachache tu, ila watoa rushwa ni Watanzania, ninawaomba katika uzee huu, bado ipo mtuombee itokomee," alisema.

"Kama huogopi, mheshimu, ukimchagua Rais wako mheshimu na namna ya kumheshimu wakati mwingine ni kumwambia ukweli, usipomwambia ukweli, utatembea unamsengenya na wanaosengenya ni wanafiki," alisema.

Aliongeza kuwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliiacha taasisi hiyo isimamie umoja na maendeleo yanayotokana na shughuli zao na utu.

# Membe: Nitakuwa Rais wa wote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, amechukua fomu kwenye Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuomba kuteuliwa kuwania nafasi hiyo, akiahidi hatakuwa rais wa wanyonge tu, bali wa Watanzania wote.

Membe, aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alifika jana kwenye Ofisi za NEC akiwa amefuatana na Mgombea Mwenza wake, Profesa Omary Fakiy Hamadi, Mwenyekiti wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu, Ado Shaibu na viongozi wengine wa chama.

Akizungumza baada ya kuchukua fomu hiyo, Membe alisema: "Mimi sitakuwa rais wa wanyonge tu, nitakuwa rais wa Watanzania wote, ili kuisaidia nchi kukua kiuchumi, iendelee na dunia ifaidi."




Mgombea Urais wa UPDP, Twalibu Ibrahim Kadege.

Membe aliendelea kusisitiza kaulimbiu ya 'Yajayo Yanafurahisha', akibainisha kuwa kilichomsukuma kugombea nafasi hiyo ni kukereketwa na dhamira yake ya kutatua matatizo ya wananchi.

Alisema Watanzania wanasubiri kwa hamu kupata Rais atakayetatua matatizo yao katika kipindi chake cha urais.

"Na mimi ni miongoni mwa watu ambao ninataka kusema wazi kabisa kilichonisukuma kugombea urais wa Tanzania ni kukereketwa kwangu na dhamira yangu ya kutatua matatizo ya wananchi. Mimi sitakuwa rais wa wanyonge tu, nitakuwa rais wa Watanzania wote," alisema.

Mgombea huyo aliahidi kuwa ACT -Wazalendo itaendesha kampeni zake kistaarabu kwa kutoa hoja za kuwashawishi wananchi waichague.

"Uchaguzi huu tutaendesha kwa ustaarabu mzuri sana na tutakuwa wastaarabu sana, tutakuwa tunakwenda na hoja za kuwashawishi Watanzania waichague ACT-Wazalendo kuchukua awamu hii ya uongozi kutoka kwa Mzee wetu John Magufuli kuileta kwa Mzee Membe ili tuweke mambo sawa.

"Hatutatukana mtu, tutaheshimu, tutakuwa tunapambana kwa hoja, kutambua kero za wananchi na namna ya kuzitatua. Ninaomba waandishi wa habari wote, hiki ni kipindi cha kusimama na kuwaeleza Watanzania msipendelee mtu mmoja, mtafanya dhambi kubwa. 'Yajayo yanafurahisha sana'," alisema.

Membe alisema mchakato wa kuwatafuta wadhamini 200 katika mikoa 10 nchini utaanza leo na kuwahakikishia Watanzania kuwa ana afya njema.

"Nitatimba nchi nzima, mikoa yote kutafuta wadhamini na wapo wengi, na kivumbi kitakapoanza rasmi tarehe 26, nitawafikia Watanzania wote popote nitakapokwenda, ningependa kusema jambo moja, uchaguzi huu ni wakipekee sana," alisema.

Akitoa maelezo kabla ya Membe kukabidhiwa fomu, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema fomu namba 8A inatumika kwa ajili ya uteuzi wa wagombea kiti cha rais na makamu wa rais ambayo imeandaliwa na tume.

"Mtawapatia seti nne ya fomu namba 8A ambayo ni fomu ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha urais na makamu wa rais na kila seti kutakuwa na nakala 10 za fomu hizo, ili kuwawezesha kujaza idadi ya wadhamini inayotakiwa," alisema.

Alibainisha kuwa watatakiwa kudhaminiwa na wapigakura wasiopungua 200 ambao wamejiandikisha kupiga kura katika kila mkoa kwenye mikoa 10 na kati ya hiyo, angalau miwili kutoka Zanzibar.

"Majina ya wadhamini katika seti zote yanatakiwa kufanana, pia mtapaswa kuwasilisha fomu za uteuzi kwa wasimamizi wa uchaguzi wa jimbo kule ambako mtaenda kutafuta wadhamini ili watoe uthibitisho kwa wadhamini hao. Tume imeshawapatia wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo yote nakala tepe na orodha ya wapigakura wa majimbo yote ili waitumie kwa kazi hiyo," alisema.

"Kutakuwa pia na tamko la kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi kwa ajili ya rais, ambapo mtapatiwa fomu namba 10, pia kutakuwa na nakala nne kwa ajili ya mgombea wa kiti cha rais na nne kwa mgombea wa kiti cha makamu wa rais."

Akikabidhi fomu, Mwenyekiti wa Tume, Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage, pia alisema katika mkoba wa fomu, kuna nakala nane za fomu namba 10 ya tamko la kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi.

"Ninawapongeza kwa kutumia haki yenu ya kuchagua na kuchaguliwa ya kikatiba na ushiriki wenu utachangia kudumisha demokrasia nchini mwetu," alisema.




Mgombea Urais wa ADC, Qeen Sendiga.

# Mgombea urais atinga NEC akiwa pekupeku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MGOMBEA wa urais kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Mutamwega Mgaywa, jana alifika kwenye Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuchukua fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea nafasi hiyo akiwa hajavaa viatu (pekupeku).

Mgaiwa alitinga katika ofisi hizo akiwa amefuatana na Mgombea Mwenza wake, Satia Musa Bebwa na viongozi wachache wa chama hicho, ambao kabla ya kuingia ukumbi wa kuchukulia fomu, walipofika walipiga magoti na kusujudu na kudai kuwa wao ni watoto wa mkulima na hawalimi wakiwa wamevaa viatu.

Akizungumza baada ya kuchukua fomu, mgombea huyo alisema kuna Watanzania wengi hadi leo hawana viatu, hivyo wao wapo pamoja na wanyonge.

"Vipaumbele vyetu ni amani, upendo na umoja na tunataka kumkomboa mkulima apate bei nzuri ya pamba kwa kilo Sh. 5,000 kulingana na soko la dunia, kahawa Sh. 5,000, korosho Sh. 5,000 ndiyo lengo letu kumkomboa mkulima.

"Tumesujudu hii ardhi kuashiria kwamba amani itatawala na kila kitu kwenye dunia ni ardhi, ardhi ndio mama wa kila kitu na Tanzania yetu tunataka ibaki na ardhi yetu kama kawaida," alisema mgombea huyo ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Mwibara mkoani Mara.




Mgombea Urais SAU, Mtamwega Mgaywa.

Mgombea Mwenza, Satia, alisema lengo lao ni kumnyanyua mkulima na kilimo kisonge mbele, akifafanua: "Tunamtaka Mrisho Mpoto kwa kuwa amekuwa akitetea wanyonge na tunataka kuungana naye."

**MGOMBEA ADC**

Naye Mgombea wa Chama cha Alliance for Democratic Change(ADC), Queen Sendiga 'Mama wa Taifa', alichukua fomu akiwa ameambatana na mgombea mwenza wake, Shoka Khamis Juma, huku wakiahidi watahakikisha huduma za afya na elimu zinatolewa bure.

**MGOMBEA UPDP**

Mgombea wa nane aliyechukua fomu jana ni wa Chama cha United People's Democratic Party (UPDP), Twalib Kadege, akiwa ameambatana na mgombea mwenza wake, Ramadhani Ali Abdallah, alisema watakwenda kutafuta wadhamini kwa matakwa ya tume.

"Kaulimbiu yetu UPDP safi na umoja daima, na tunaamini umoja utawezesha kupata kiti cha urais, tumejipanga kwa hilo, tukimaliza taratibu za kusaka wadhamini, ndiyo tutasema vipaumbele vyetu, na utafutaji wa wadhamini tutaanzia Dodoma na tunaamini wagombea wetu watachaguliwa na tutapata wabunge wengi," alisema Kadege.

HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi Taifa, James Mbatia, akifungua Mkutano Mkuu wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana.
PICHA: MIRAJI MSALA

# Serikali yavunja rekodi ukuaji uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeendelea kuvunja rekodi ya ukuaji wa uchumi wa nchi katika kipindi cha miaka minne ya awamu ya tano sambamba na kupunguza mfumuko wa bei kutoka wastani wa asilimia 9.2 mwaka 2015 hadi asilimia 4.3 mwaka 2019/20.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, aliwaambia waandishi wa habari jana jijini hapa kuwa sasa Pato la Taifa (GDP) ni kubwa kuliko miaka yote tangu uhuru.

Alisema hatua hiyo imesababisha kufanya uchumi wa Tanzania kuwa wa 10 barani Afrika na mfumuko wa bei kuwa mdogo kuliko wakati wowote katika historia ya Tanzania.

"Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano, Pato la Taifa limekua kwa wastani wa Sh. trilioni 124 kwa mwaka ikilinganishwa na wastani wa Sh. trilioni 52.9 kwa mwaka katika kipindi cha awamu ya nne," alisema Dk. Abbasi ambaye ni Msemaji Mkuu wa Serikali.

Kwa mujibu wa Dk. Abbas, serikali imesimamia na kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa na ukuaji mzuri wa uchumi na kwamba katika miaka minne (2016-2019) uchumi wa Tanzania umekua kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa mwaka, wastani ambao ni mkubwa ikilinganishwa na awamu zote.

Dk. Abbas alisema msingi mwingine muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi na katika kutekeleza azma ya kujitegemea umekua kuongeza mapato ya serikali kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 mwaka 2015 hadi Sh. trilioni 1.3 mwaka 2016, 2018/19 na Julai, 2019 hadi Juni, mwaka huu, umefikia wastani wa Sh. trilioni 1.5 ambapo kwa Desemba, mwaka jana na Juni, mwaka huu zimekusanywa Sh. trilioni 1.9 mtawalia.

Pia alisema serikali imeongeza mapato yasiyo ya kodi kutoka Sh. bilioni 688.7 mwaka 2014/15 hadi Sh. trilioni 2.4 mwaka 2018/19.

Alisema kuongezeka kwa mapato hayo, ni matokeo ya kubana mianya ya kukwepa kodi, mwamko wa wananchi kulipa kodi, usimamizi mzuri wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlala ya Mapato Tanzania (TRA) na serikali kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, Dk. Abbasi alisema kuwa taasisi za kimataifa zimeendelea kusifia ukuaji wa uchumi wa nchi na Septemba 30, mwaka jana, Benki ya Dunia iliitaja Tanzania kuwa ni nchi yenye uchumi unaokua kwa wastani wa asilimia sita hadi saba kwa mwaka katika kipindi cha miaka 10.

"Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeitaja Tanzania kuwa nchi yenye uchumi jumuishi wenye kuzingatia maslahi ya umma, uwekezaji imara na unaokuwa pamoja na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za nje.

"Aidha, Machi, mwaka huu, Shirika la Fedha Duniani (IMF) limesema hali ya uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara ukikua kwa zaidi ya asilimia 6, mfumuko wa bei ukiwa chini ya asilimia tano na akiba ya fedha za kigeni ikiwa ya kutosheleza na deni la taifa likiwa himilivu," alisema Dk. Abbasi.

Pia alisema jarida la Forbes linaitaja Tanzania kuwa nchi ambayo uchumi wake umekua kwa wastani wa asilimia sita hadi asilimia saba kwa mwaka kutokana na matumizi mazuri ya rasilimali zake na utalii kati ya mwaka 2009 hadi 2017.

# Ajali ya gari yaua wanafunzi watatu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAFUNZI watano wa Shule ya Sekondari Olmoti mkoani Arusha, wamepata ajali na watatu kati ya hao wamefariki dunia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salum Hamduni, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 11:30 jioni katika barabara ya Afrika Mashariki eneo la Olmoti, Wilaya ya Arusha.

Aliwataja waliofariki dunia katika ajali hiyo, Christina Mkondola (16) mwanafunzi wa kidato cha kwanza, Rebeca Msengi (16) wa kidato cha pili na Ben Naiman (15) mwanafunzi wa kidato cha kwanza. Alisema wote hao walifariki dunia katika eneo la tukio.

Kamanda Hamduni aliwataja majeruhi wa ajali hiyo kuwa ni Elevira Epodi (16) na Shamira Nkini (14) wote wanafunzi wa kidato cha kwanza na wanaendelea na matibabu Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mount Meru.

Alisema siku ya tukio, gari lenye namba T.768 BKL aina ya Jeep lililokuwa likiendeshwa na Sariko Mwenda (64) liliacha njia na kuwagonga wanafunzi hao waliokuwa wakitembea kwa miguu.

"Ajali hiyo imetokea wakati gari hilo likitokea Usa River kuelekea mzunguko wa Kisongo. Dereva aliwagonga watembea kwa miguu hao ambao wote ni wanafunzi wa shule hiyo na walikuwa upande wa kushoto wakitokea shuleni kuelekea nyumbani kwao," alisema.

Alitaja chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva huyo kuendesha gari kwa mwendokasi na kujaribu kuyapita magari mengine yaliyokuwa mbele yake na kushindwa kulimudu gari.

Kamanda Hamduni alisema baada ya dereva huyo kupoteza uelekeo, aligonga gari lililokuwa ubavuni mwake lenye namba za usajili T.251 AJB aina ya Toyota Hilux Double Cabin na baiskeli moja.

Hamduni alisema mtuhumiwa amekamatwa na atafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika.

Alitoa wito kwa madereva kuchukua tahadhari pindi wanapotumia vyombo vya moto na kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu za usalama wa barabarani ili kuepusha ajali zisizo za lazima. Alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mount Meru kusubiri taratibu za mazishi.

# Ujenzi SGR wamkuna PM

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alikagua ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) na kueleza kuwa ameridhishwa na kasi ya maendeleo ya kazi hiyo ambayo imefikia asilimia 87 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro.

Amesema serikali imedhamiria kuimarisha miundombinu ya usafiri wa reli, anga, maji na barabara ili kutoa fursa kwa wananchi kuchagua aina ya usafiri wanaohitaji kuutumia pia kukamilika kwa mradi huo kutaimarisha biashara baina ya Tanzania na mataifa mengine.

Majaliwa ambaye alianza ziara hiyo kwa kukagua ujenzi wa jengo la stesheni ya Dar es Salaam ambalo lina mwonekano wa madini ya tanzanite, alisema ujenzi unaendelea vizuri na amemtaka mkandarasi akamilishe kwa wakati kwa kuwa Watanzania wanasubiri kwa hamu.

"Hii ni mara yangu ya tatu nafanya ukaguzi wa ujenzi wa mradi huu na wakati wote naridhishwa na maendeleo ya ujenzi wake ambao unajengwa kwa kutumia fedha za Watanzania na asilimia 90 ya wafanyakazi wanaojenga mradi huu ni Watanzania," alisema.

Waziri Mkuu alisema Watanzania waendelee kuiamini serikali yao kwa sababu imejipanga katika kuendelea na kuimarisha ujenzi wa miradi mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Akiwa katika stesheni ya Ruvu mkoani Pwani, Waziri Mkuu alipokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi yakiwamo ya wakulima kunyanyaswa na wafugaji kwa kuingiza mifugo katika mashamba yao, hivyo kuwafanya wakose chakula.

Pia wananchi hao ambao baadhi yao maeneo yao yalitwaliwa kupisha ujenzi wa mradi wa SGR, walisema wamehamia kwenye maeneo ambayo hayana miundombinu ya maji. Kutokana na malalamiko hayo, Waziri Mkuu alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, leo aende na wataalamu wake wakasikilize kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, alisema mafanikio yanayoonekana katika mradi huo ni matokeo ya kazi kubwa inayofanywa na serikali ya awamu ya tano.

Alisema mkandarasi anayejenga mradi huo, kampuni ya Yapi Merkezi, ameanza kufanya majaribio ya kupitisha treni za kihandisi katika baadhi ya vipande kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro.

Mhandisi Nditiye alisema licha ya ujenzi wa mradi wa SGR pia Shirika la Reli Tanzania (TRL) linatekeleza mradi wa uboreshaji wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Isaka na kazi hiyo imefikia asilimia 93 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Tabora na unatarajiwa kukamilika Februari 2021.

# TPSF yaomba kushiriki vita ujangili

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), imesema serikali inatakiwa kushirikiana nao katika mapambano dhidi ya ujangili badala ya kuwategemea wadau wa maendeleo katika kutatua tatizo hilo.

Rai hiyo imetolewa na Mwakilishi wa TPSF, Victoria Michael, akitoa mada kwenye mkutano wa mafunzo kwa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) yaliyofanyika kwa njia ya mtandao chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID). Alisema mapambano dhidi ya ujangili yamekuwa yakifanywa kwa kiasi kikubwa na serikali, huku sekta binafsi ikiachwa nyuma, hivyo kuna haja ya wao kushirikishwa.

"Sekta binafsi ziliachwa nyuma, tunaona serikali pekee ipo na wadau wa maendeleo utakuta wale ambao wanawinda mnyama akishaua, atasafirisha kwa barabara, wapo ambao watafanya biashara hiyo haramu halafu ile fedha itarudi kwenye mzunguko. Kwa hiyo, hapo waliopo katika huo mzunguko ni sekta binafsi," alisema.

Michael alisema unapoiacha sekta binafsi kisha unaelezea wanyamapori, ni kama unajaribu kuelezea tatizo bila kwenda kwenye chanzo. Alisema wamekuwa wakifanya semina mbalimbali kwa kuwaelimisha watu wote wa sekta binafsi kuhusiana na umuhimu wa wanyamapori na uhifadhi wa mazingira.

Alisema bado kuna kazi kubwa ya kuwaelimisha hata walivyotuma mialiko ya kuwaita kwenye mikutano, walijiuliza wao wanashiriki kwa ajili ya kitu gani.

Alisema kuna jitihada mbalimbali ambazo sekta binafsi wamekuwa wakizifanya ingawa hazionekani, hivyo mchango wao umekuwa mdogo.

Michael alisema sekta binafsi imeanzisha kamati ambayo itafanya kazi kwa miaka mitano kusaidia kutatua matatizo kwenye sekta ya uhifadhi wa mazingira na wanyamapori.




Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu Serikali ya Awamu ya Tano kuvunja rekodi ya ukuaji wa uchumi wa nchi katika kipindi cha miaka minne ya utawala wake, sambamba na kupunguza mfumuko wa bei kutoka wastani wa asilimia 9.2 mwaka 2015 hadi asilimia 4.3 mwaka 2019/2020. **PICHA: MAELEZO**

# Makatibu wakuu wanachama SADC wajadili mpango mkakati kwa video

**Na Mwandishi Wetu**

MAKATIBU Wakuu kutoka Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wamekutana na kujadili rasimu ya mpango mkakati elekezi mpya wa maendeleo wa kanda (2020 - 2030) na rasimu ya dira ya SADC (2020 - 2050) kwa njia ya video jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana baada ya kumalizika kwa mkutano huo, Mwenyekiti wa makatibu wakuu hao, ambaye Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na UShirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, alisema lengo lilikuwa kuangalia dhima ya SADC kuanzia sasa 2020 hadi 2050 na mpango mkakati wa SADC kuanzia mwaka 2020 - 2030 kwa sababu mpango mkakati wa SADC uliokuwa unatumika tangu mwaka 1992 umekwisha muda wake.

"Nyaraka hizi mbili ni za muhimu sana kwa sababu hadi sasa hivi toka SADC ilipoanzishwa mwaka 1992 imefanya mambo makubwa, lakini sasa ule mpango mkakati wake uliokuwa unatumika tangu mwaka 2010 na ambao ulihuishwa mwaka 2015, umeisha muda wake, hivyo ilikuwa muhimu sana kuandaa rasimu ya nyaraka hizi muhimu," alisema.

Aliongeza kuwa rasimu za nyaraka hizo mbili zitawasilishwa kwenye mkutano wa 40 wa wakuu wa nchi wanachama wa SADC na serikali unaotarajiwa kufanyika Agosti 17, mwaka huu, kwa njia ya mtandao.

Mkakati wa SADC ni mpango wa maendeleo ya kanda uliopitishwa na mkutano wa wakuu wa nchi na serikali uliofanyika mwaka 2003 jijini Dar es Salaam na ulianza kutekelezwa rasmi mwaka 2005 kwa kipindi cha miaka 15 tangu mwaka 2005.

Aidha, mpango huo una vipaumbele vinne ambavyo ni maendeleo ya viwanda na mtangamano wa soko, miundombinu bora, amani na usalama, pamoja na programu maalum.

"Dira ya SADC 2020 - 2050 inatoa taswira ya jumuiya kwa miaka 30 ijayo ambapo msingi wake ni amani, ulinzi, utulivu na utawala bora, uchumi wa kati unaoendeshwa na sekta ya viwanda na wanajumuiya wenye hali bora ya maisha," alisema Balozi Ibuge.

Kutokana na hali hiyo, alisema dira ya SADC 2050 ni muhimu kwa maendeleo ya ukanda wa kusini mwa Afrika hususan katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030 na ajenda ya Umoja wa Afrika ya Mwaka 2063.

Katika tukio jingine, Balozi Ibuge alikutana na kufanya mazungumzo na Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) nchini Tanzania, Antonio Canhandula, katika ofisi ndogo za Wizara jijini Dar es Salaam.

Balozi Ibuge alisema UNHCR imekuwa na mchango mkubwa sana unaohusisha kulinda haki za wakimbizi, lakini kuwarejesha wakimbizi nchini mwao.

Pamoja na mambo mengine, mazungumzo yalilenga kuimarisha uhusiano baina ya Tanzania na UNHCR kwa ujumla.

# Kampuni yazoa tuzo za utalii

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KAMPUNI ya Coastal Aviation, imetwaa tuzo mbili katika hafla ya utoaji wa tuzo za utalii zilizoandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) jijini Arusha juzi.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo ilifanyika chini ya Waziri Dk. Hamis Kigwangalla, aliyekuwa mgeni rasmi, zikishirikisha makundi 32 ya wadau wa sekta hiyo nchini.

Coastal ilitangazwa mshindi katika kundi la mwendeshaji bora wa usafiri wa anga ukanda wa utalii wa Kaskazini pamoja na ule wa Kusini kwa mwaka 2017/18.

Kampuni hiyo pia ilitangazwa kung'ara katika kuisaka kampuni bora ya ndege ukanda wa Serengeti katika tuzo hizo za TANAPA.

"Tumefurahi kupata tuzo hizi na kutambuliwa kwa kazi nzuri na usafiri wetu wa kuaminika nchini. Huu ni mwaka ambao pia tulizindua kampeni yetu ya 'Fly Green', ambayo imekuwa na mafanikio makubwa.

"Tunawakaribisha kufurahia huduma zetu, tukiamini zaidi katika usalama na mazingira mazuri na ya uhakika wa safari kwa wateja wetu. Hata katika kipindi hiki cha tisho (la corona), wateja wetu tunawahakikishia usalama dhidi ya tatizo hilo.

"Tunawashukuru wateja wetu, mawakala, TANAPA, Wizara ya Maliasili na Utalii na wengine wengi kwa kutuamini na kutuunga mkono; hakika isingewezekana bila ninyi," alisema Rubani Maynard, aliyeiwakilisha kampuni hiyo katika tuzo hizo jijini.

Waziri Kigwangalla alitumia fursa hiyo kuwataka wadau wa sekta ya utalii kuendelea kutumia mbinu zote muhimu za kijikinga na maambukizi ya corona kwa faida ya biashara ya utalii, lakini kwa serikali kupata mapato.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Alyoce Nzuki, alisema anatambua mchango mkubwa wa wadau hao katika sekta ya utalii na kwamba ofisi yake itaendelea kushirikiana nao kila hatua.

Mwenyekiti wa Bodi ya TANAPA, Jenerali mstaafu George Waitara, alisema sekta ya utalii nchini ni muhimu kwa kuwa inachangia pato la taifa kwa asilimia 17 na fedha za kigeni kwa asilimia 25.



Kaimu Meneja Msaidizi Idara ya Forodha wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Paul Kamkulu (wa nne kulia), akiwatambulisha watumishi wa TRA wa Kituo cha huduma kwa pamoja mpakani cha Namanga mkoani Arusha, kwa Mwenyekiti wa Bodi ya mamlaka hiyo, Dk. Suleiman Missango (wa pili kushoto) pamoja na Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede (mwenye tai nyekundu nyuma), na wajumbe wengine wa bodi, walipotembelea kituoni hapo, mapema wiki hii, kujionea namna shughuli za forodha zinavyofanyika. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mfugaji aliyedaiwa kuuawa na askari TANAPA azikwa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MFUGAJI Ulandi Dotto (28) mkazi wa Kijiji cha Mwanavala, Mbarali mkoani Mbeya, anayedaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi na askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) wakati akipitisha mifugo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, amezikwa huku wafugaji wakishauriwa kutolipa kisasi.

Wafugaji pia wameombwa kutoichukia TANAPA kwa madai kuwa askari wanaodaiwa kufanya mauaji hao ni wahalifu kama wahalifu wengine na kwamba vyombo vya dola vinalishughulikia suala hilo.

Akizungumza wakati wa maziko ya kijana huyo yaliyofanyika kijijini kwao, Mwanavala Kata ya Imalilo - Songwe wilayani Mbarali, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Taifa, John Wambura, alisema chama hicho kitahakikisha haki inatendeka. Wambura alisema akiwa kiongozi mkuu wa chama hicho, hatakuwa tayari kushuhudia wafugaji wakilipa kisasi dhidi ya askari waliotekeleza tukio hilo badala yake kila mmoja atatakiwa kuzingatia sheria. "Mmesema hapa kwamba tukio hili ni la tano kutokea katika wilaya hii. Tunajua hakuna fidia ya uhai wa mwanadamu, lakini angalau serikali itoe kifuta machozi. Niwahakikishie kwamba hawa maaskari (askari) lazima mtawaona mahakamani," alisema Wambura.

Alisema viongozi wa juu wa chama cha wafugaji nchini watahakikisha wanashirikiana na familia ya marehemu kuhakikisha haki inatendeka na familia inapata haki yake.

Baba mzazi wa marehemu, Mzee Dotto Shigela, aliwaomba wadau mbalimbali kumsaidia ili familia yake ipate haki kwa madai kuwa mtoto wake ameacha mke na watoto wawili ambao watahitaji kupata malezi bora.

Alisema Ulandi ndiye alikuwa mtoto wake wa kwanza na alikuwa msaada mkubwa kwenye familia, hivyo akadai kuwa maisha ya wanafamilia hao yatayumba kutokana na kutokuwapo kwake.

"Nililalamika kwa RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa) maana walianza kupindisha wakati tunaandikisha. Walianza kudai kuwa risasi iliingilia kifuani wakati ukweli ni kwamba risasi iliingilia mgongoni na ikatokea kifuani, hivyo naomba sana haki itendeke kwenye tukio hili," alisema Shigela.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambaye ni Ofisa Mifugo wa Wilaya hiyo, Augustino Lawi, alisema serikali inawathamini na inahitaji mifugo iendelee kustawi kutokana na kuwa miongoni mwa sekta zinazoiingizia mapato mengi.

Lawi alisema sekta ya mifugo ni ya pili kwa kuiingizia mapato halmashauri hiyo baada ya kilimo. "Tatizo ni kwamba ufugaji wetu utategemea sana malisho ya asili kama wanyama wengine hali ambayo imekuwa ikisababisha migogoro. Sasa hivi tuna dhamira ya kubadili ufugaji kwa kuanza kuzalisha malisho ili tuondoe huu uhaba wa malisho," alisema Lawi.

Mwanasheria wa chama cha wafugaji nchini, Glorious Luoga, aliwataka wafugaji kuhakikisha wakati wanadai haki, pia wazingatie sheria za nchi ili kuepuka migogoro isiyo na ulazima. Alisema moja kati ya taratibu wanazostahili kuzingatia ni kuepuka kuingiza mifugo kwenye hifadhi na kwamba ni wajibu wa wafugaji kuzingatia utaratibu huo na kwamba hakuna haki bila wajibu.

# Corona ilivyobadili utendaji mashirika

**Na Enock Charles**

MLIPUKO wa virusi vya corona umesababisha madhara makubwa duniani kote, huku ukielezwa kuleta mabadiliko katika utendaji wa mashirika na taasisi.

Kutokana na ugonjwa huo kuambukizwa kwa hewa, mikutano ya ana kwa ana sasa ilihamia kwenye mitandao ya jamii ukiwamo mtandao maarufu wa Zoom.

Katika mkutano uliofanyika hivi karibuni kupitia mtandao huo, ukiandaliwa na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WTF), baadhi ya wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali, akiwamo Mkurugenzi wa Mtandao wa Kijinsia (TGNP), Lilian Liundi, walizungumzia athari za ugonjwa huo na mkakati waliouweka ili kuendeleza majukumu yao.

"Baada ya Tanzania kutangaza uwapo wa corona (Machi 16 mwaka huu), taasisi ilikuwa na mikutano mingi mikubwa, ila hatua ya kwanza ilikuwa ni kuisitisha na kuwapa taarifa washiriki.

"Lakini kwa haraka tuliunda kamati ya kupambana na janga hili ili kuhakikisha kila kitu kinaendelea," alisema Liundi.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi ilinunua jukwaa la mtandaoni ili kuwezesha kufanya vikao kama kawaida, mabadiliko yaliyofanyika kwa haraka. "Kila changamoto ina fursa zake na pia ina jambo la kujifunza. Baada ya janga hili kutokea nchini, mashirika mengi yamejifunza namna ya kukabiliana na milipuko kama hiyo," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Jitihada za Maendeleo, Janet Mawinza, alisema janga la corona lilileta shida ufanyaji shughuli za utetezi wa kinamama na watoto.

"Mwezi ule wa tatu (Machi), tulianza kampeni ya kumlinda mtoto wa kike kwenye masuala ya ngono kabla ya umri. Wakati tupo kwenye mchakato, corona iliingia nchini, kwa hiyo shughuli zote ilibidi zisimame," alisema na kubainisha kuwa baadaye walianza utaratibu wa kufanyia kazi nyumbani na kila kitu kilienda sawa.

Mkurugezni wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya, alisema japo kwa Tanzania hakukuwa na hofu kubwa ya corona, athari za ugonjwa huo zilikuwa kubwa kiutendaji.

Alisema walishirikiana na mashirika mengine ili kutengeneza mpango wa dharura wa kukabiliana na ugonjwa.

"Sisi tuliandaa chumba, ikitokea mtu amepata shida tunamweka huko. Tuliona kuna haja ya kufanya zuio la watu kuja ofisini, ili kupunguza maambukizi," alisema.

# Kortini madai ya kukutwa na tausi

**Na Hellen Mwango**

RAIA sita wa China wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ikiwamo kuongoza genge la uhalifu na kukutwa na nyara za serikali ndege aina ya tausi isivyo halali.

Washtakiwa hao ni wafanyabiashara Jin Erhao (35), Chengfa Yang (49), Ren Yuangqing (55) Mkurugenzi wa Kampuni ya Usafirishaji ya Sinota, Shu Nan (50), mfanyakazi katika kampuni hiyo, Chen Shinguang (45) ambaye ni meneja wa kampuni hiyo na Meneja Ufundi wa kampuni hiyo, Gu Jugen (57).

Mapema juzi, washtakiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na mawakili wa serikali, Salim Msemo na Elia Athanas na utetezi uliongozwa na Wakili Ibrahim Bendera.

Wakili Msemo alidai kuwa katika shtaka la kwanza, washtakiwa wanadaiwa kuongoza genge la uhalifu na kwamba Agosti Mosi, mwaka huu, mtaa wa Sokoine, jijini Dar es Salaam, wote kwa pamoja na kwa makusudi walisimamia genge la uhalifu lililosababisha kupatikana kwa tausi mmoja mwenye thamani ya dola za Marekani 500 sawa na Sh. 1,155,000 za Tanzania kinyume cha Sheria ya Wanyamapori.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Agosti Mosi, mwaka huu, mtaa wa Sokoine, washtakiwa hao walikutwa na tausi mmoja mwenye thamani ya Sh. 1,155,000 kinyume cha Sheria ya Wanyamapori.

Aliendelea kudai kuwa katika shtaka la tatu, washtakiwa hao wanakabiliwa na shtaka la kukutwa na nyara za serikali ambayo ni tausi mmoja mwenye thamani ya Sh. 1,155,000 kosa wanalodaiwa kulitenda Agosti Mosi, katika mtaa wa Sokoine, jijini Dar es Salaam.

Baada ya kuwasomea mashtaka, Wakili Msemo alidai upelelezi wa shauri hilo haujakamilika na upande wa Jamhuri haukuwa na pingamizi la dhamana, lakini waliomba masharti yawe makali kulingana na mashtaka yalivyo.

Akitoa masharti ya dhamana, Hakimu Kabate aliwataka washtakiwa hao kila mmoja kupeleka wadhamini wawili wa kuaminika walio ndani ya Mamlaka ya Mahakama (ndani ya mkoa wa Dar es Salaam na Pwani) watakatiaosaini bondi ya Sh. 500,000 kila mmoja.

Pia aliwataka kuwasilisha pasi zao za kusafiria mahakamani na kutakiwa kutokusafiri nje ya mkoa wa Dar es Salaam bila ruhusa ya mahakama.

Wakili wa utetezi, Bendera, alidai kuwa pasi za kusafiria za washtakiwa hao kwa sasa zinashikiliwa na polisi, hivyo uwezekano wa kuziwasilisha kwa wakati haukuwapo. Hakimu Kabate alimtaka kuwasilisha uthibitisho iwapo ni kweli pasi hizo ziko mikononi mwa polisi.

Aliwataka mawakili wa pande zote kushirikiana kupata uthibitisho huo ili kuwapatia washtakiwa dhamana.

"Wakili Msemo mnaweza kushirikiana kupata uthibitisho hata kwa simu. Mimi nipo mkipata uthibitisho tutakamilisha dhamana, lakini kwa sasa washtakiwa watabaki mahabusu mpaka tupate uthibitisho," alisema Hakimu Kabate.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu, wachezaji waheshimu mikataba kuepusha mvutano

**KLABU** za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili, tayari zipo mawindoni kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao kuelekea msimu mpya unaotarajiwa kuanza mapema mwezi ujao.

Ligi Kuu ndiyo itakayokuwa ya kwanza kuanza kutimua vumbi katika viwanja 18 nchini hapo Septemba 6, mwaka huu kabla ya ligi hizo nyingine kuanza, na tayari klabu zimeshaanza kusajili baada ya dirisha kufunguliwa tangu Agosti Mosi mwaka huu, huku likitarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi huu.

Tunatoa pongezi kwa klabu ambazo tayari zimetangaza mapema wachezaji isiyowahitaji kuelekea msimu mpya, hivyo kuwapa nafasi ya kutafuta timu nyingine kabla ya dirisha hilo kufungwa, hivyo zile ambazo hazijafanya hivyo, tunasisitiza kuzingatia hilo mapema.

Hata hivyo, kanuni na umakini zaidi kwa klabu na hata wachezaji unahitajika hususan kwa kulinda mikataba yao kwa wale ambao wameshaingia ama wanatarajiwa kuingi ili kuepusha migogoro kati ya pande husika.

Tunatoa tahadhari hiyo hasa kwa kutambua kwamba ni nadra sana kwa dirisha la usajili Tanzania Bara kumalizika bila kusikia mvutano kwa klabu na klabu ama klabu, mchezaji na klabu nyingine kuvutana kuhusu kusajili mchezaji wao kinyume cha taratibu.

Hivyo, hatutaki kusikia ama kuona mchezaji akilazimika kufungiwa ama kupotezewa muda wake wa kushuka dimbani kutokana na ukiukwaji huo wa kanuni ambao unaweza kuepukika.

Miaka iliyopita tulishuhudia mivutano kama hiyo kwa mchezaji kama Athumani Iddi 'Chuji' katika usajili wake wa kutoka Simba kwenda Yanga, lakini Ramadhani Singano kutoka Simba kwenda Azam FC.

Hao ni baadhi tu ya wachezaji ambao sakata lao la usajili lilifikia hatua hadi wachezaji kudai mikataba na saini zao zimeghushiwa hatua iliyosababisha kufikishana katika vyombo vya dola.

Kadhalika, tulishuhudia pia mchezaji wa Mbao FC, Pius Buswita, akijisajili klabu mbili tofauti jambo ambalo Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilichukua hatua ya kumfungia kucheza soka kwa kipindi cha mwaka mmoja kutokana na kosa hilo, adhabu ambayo hatutaki kuona ikitokea tena kwani inadumaza kiwango cha mchezaji husika na kumpotezea mipango yake kisoka.


Hata hivyo, tunasikitishwa na mvutano ambao unaendelea kati ya Yanga na kiungo mshambuliaji wao raia wa Ghana, Bernard Morrison ambaye amedai saini yake imeghushiwa katika mkataba mpya ambao anadaiwa kuingia na klabu hiyo baada ya ule wa miezi sita kumalizika.

Hayo yote yakihusishwa na tetesi za Simba kumtaka mchezaji huyo, kimsingi Nipashe hatuegemei upande wowote, kwani tunahitaji kuona suala hilo likimalizwa kwa kufuata kanuni na pande zote zikiridhika kwa uamuzi utakaochukuliwa bila kuonewa.

Misimu iliyopita tulifurahishwa na namna kiungo Mnyarwanda Haruna Niyonzima, na mshambuliaji mzawa, Ibrahim Ajibu baada ya kumaliza mikataba yao kwenye timu zao wakiruhusiwa kuondoka bila mvutano, awali Ajibu akitoka Simba kwenda Yanga kabla ya kurejea tena huku Niyonzima naye akitoka Yanga na kutua Simba kabla ya kutoka na kurejea tena, hicho ndicho tunachotaka kukiona na si hili la Morrison kwa sasa.

Kimsingi katika kipindi kama hiki cha dirisha la usajili, ndicho cha mavuno kwa wachezaji kwa kujiingizia mamilioni ya fedha pale wanaposaini mikataba mipya kwenye timu zao au wanazohamia, hivyo klabu zisiwaharibie kwa sababu soka ni maisha yao na wachezaji nao wanapaswa huheshimu mikataba yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kongole Simba, heko Namungo

**NALAZIMIKA** kuwapa kongole (shukrani; asante) viongozi wa Simba kwa jinsi walivyoiongoza timu yao na kukamilisha msimu uliomalizika hivi karibuni kwa kutwaa vikombe viwili na ngao mfululizo.

Naam, "Anayejitahidi hufaidi." Maana yake yeyote anayetia bidii hufaidi kutokana na juhudi zake. Hii ni methali inayowanasihi watu kuwa na bidii katika shughuli yoyote wafanyayo. Ndivyo walivyofanya viongozi wa klabu ya Simba, wachezaji, wanachama na mashabiki waliojaa uwanjani kuwashajiisha (kuwahamasisha; kuwapa ari) wachezaji wakati timu yao ilipocheza nyumbani na ugenini.

Kwanza Simba ilitwaa Ngao ya Jamii kwa kuifunga Azam mabao 4-2 kisha Kombe la Ligi Kuu ya Tanzania Bara kwa mara ya tatu mfululizo wakipata alama 88. Yanga iliambulia nafasi ya pili kwa kupata alama 72 ikipitwa kwa alama 16 na Simba, kisha Azam iliyopata alama 70 ikiachwa na Simba kwa alama 18.

Kama haitoshi, Simba wakatwaa Kombe la Shirikisho (ASFC) kwa kuifunga timu ngeni ya Ligi Kuu, Namungo FC kwa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

Hii yanikumbusha methali isemayo "Penye nia pana njia." Maana yake ikiwa mtu ana dhamira ya kufanya jambo fulani hawezi kukosa njia. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba tuwapo na nia ya kufanya jambo, lazima tufanikiwe.

Viongozi wa Simba wakiongozwa na MO Dewji walikuwa na nia; hivyo wamevuna walichopanda. Najikalifisha (kitendo cha kujilazimisha kutenda jambo), kuwapa Simba kongole kwa mara nyingine, ingawa naumia ndani kwa ndani!

Nakiri walivyosema wahenga kuwa: "Kweli ingawa chungu niambie sinifiche." Twafunzwa umuhimu wa kuwa na tabia ya kuusema ukweli au kuwa watu wausemao ukweli.

Kama kumbukumbu zangu si sahihi, natangulia kuomba radhi, lakini kama ni sahihi, nathubutu kusema Simba imeweka rekodi ya pekee kwa kutwaa vikombe viwili na ngao kwa msimu mmoja. Wahenga walikuwa sahihi walipokuwa: "Anayejitahidi hufaidi." Maana yake anayetia bidii hufaidi kutokana na juhudi zake. Hii ni methali inayowanasihi watu kuwa na bidii katika shughuli wafanyazo.

Mafanikio ya klabu ya Simba yapaswa kuwa mfano kwa timu zingine. Sio zinazoshiriki Ligi Kuu tu, bali timu zote za kandanda nchini. Mchezo wa kandanda unapendwa sana nchini kama unavyopendwa duniani kote, lakini twashindwa kuwaendeleza wachezaji wetu kwani twawategemea mno wachezaji wa nje wanaokuja kuchuma kwetu na kujinufaisha huko watokako! Tutazinduka lini?

Funzo kubwa kwa klabu nyingine ni kuwa makini, kufanya usajiri wa kimya kimya, kujiepusha na uropokaji wa kuweka hadharani kila kinachokusudiwa kufanywa na klabu husika. Maana yangu ni kusajili wachezaji kimya kimya badala ya kutangaza majina ya wachezaji wanaokusudiwa.

Sitafanya haki kukamilisha makala yangu bila kuipongeza timu ya Namungo iliyoingia Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu uliopita na kushika nafasi ya nne chini ya Simba, Yanga na Azam kwa mtiririko huo. Pia imeweza kuingia fainali ya Kombe la Shirikisho ilipofungwa 2-1 na Simba kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

Wachezaji wasajiliwe kwa umahiri wao, si majina. Aidha, wawe wamechunguzwa tabia au mienendo yao nje na ndani ya uwanja. Wasichaguliwe kwa kuwa walizifunga timu za Azam, Simba na Yanga tu. Kadhalika, wachunguzwe nidhamu, yaani mpangilio maalumu wa kufanya jambo; adabu mbele ya watu wengine.

Pia matendo yao wanapokuwa mitaani kama wana uraibu (wa kuvuta sigara, bangi, dawa za kulevya na uasherati) au la. Wachezaji wenye tabia hizo hawafai.

Baada ya kuchunguza yote hayo na kufanya usajili, klabu zapaswa kuwa na utaratibu wa kulipa mishahara ya wachezaji kila mwezi kama ilivyo sheria. Mishahara ya wachezaji inapocheleweshwa huwakatisha tamaa hivyo kucheza chini ya viwango na kutowaheshimu viongozi na walimu wao.

Wachezaji wa kigeni wanaocheza nchi za nje hulipwa mishahara mikubwa inayozidi baadhi ya marais wetu wa Afrika na kwingineko duniani. Mishahara wanayolipwa wachezaji hao, kwa mfano Christiano Ronaldo, Lionel Messi, Mohamed Salah, n.k. ni mikubwa.

Hii ndio inayowapa jeuri ya kununua ndege (eropleni) zao binafsi, meli, majumba ya fahari yenye gharama kubwa na msururu (vitu vilivyokaa kimoja baada ya kingine; msogo) wa magari ya aina tofauti.

Hapa Tanzania wachezaji husajiliwa kwa kulipwa milioni kadhaa za fedha na mishahara mikubwa kuliko idadi kubwa ya wafanyakazi! Hata hivyo inasikitisha kwani wanashindwa kutambua umuhimu wao kwa taifa!



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (wa nne kulia) na ujumbe wake, wakipata maelezo kutoka kwa Mtaalam wa Sayansi ya Udongo na Uzalishaji Mazao wa kiwanda cha Kagera Sugar, Geofrey Semakula (kushoto) kuhusu matumizi ya vifaa vya kisasa katika kilimo cha miwa, walipotembelea kiwanda hicho mkoani Kagera mapema wiki hii, kwa lengo la kusaidia uwekezaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafikishwa kortini kesi uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

WATU wanne wakiwamo raia wawili wa Kenya, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuisababisha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), hasara ya Sh. milioni 16.6.

Washtakiwa hao ni, Beth Ngunyi (43) mfanyabiashara na mkazi wa Kasaram, Nairobi nchini Kenya, Frolence Dirango (34) mfanyakazi wa Kampuni ya Betlee kama Ofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Alven Swai (26) mkazi wa Mbezi Beach na Godluck Macha (28) mfanyabiashara na mkazi wa Mbezi Beach.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Luboroga, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo.

Wakili wa Serikali, Batilda Mushi, alidai kuwa kati ya Julai Mosi na Julai 26, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali, washtakiwa kwa pamoja walikula njama ya kutumia vifaa vya mawasiliano.

Alidai kuwa Julai 13, mwaka huu, maeneo ya Tarakea, Rombo mkoani Kilimanjaro, Ngunyi na Dirangu waliingiza vifaa vya kielektroniki nchini pasipo kuwa na leseni ya TCRA.

Mushi alidai Julai 20, mwaka huu, maeneo ya Kibona Lodge Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao walisimika vifaa vya mawasiliano bila kuwa na leseni kutoka TCRA.

Katika mashtaka ya nne, inadaiwa kati ya Julai 20 na 26, mwaka huu, maeneo ya Kibona Lodge, kinyume cha sheria walifanyia marekebisho ya vifaa hivyo vya kielektroniki.

Pia inadaiwa kinyume cha sheria, washtakiwa hao waliendesha mitambo ya mawasiliano bila kuwa na leseni.

Mushi alidai washtakiwa hao, kinyume cha sheria, walitumia vifaa vya mawasiliano vilivyounganishwa na vifaa vingine vya mawasiliano kwa nia ya kupokea na kusambaza mawasiliano bila kupata uthibitisho wa TCRA.

Washtakiwa hao wanadaiwa walikwepa kufanya malipo ambayo yalipaswa kufanyika kwa kuruhusu mawasiliano nje ya nchi kutokana na kutumia kifaa hicho cha mawasiliano bila kuwa na leseni.

Katika mashtaka ya tisa, inadaiwa Julai 13, mwaka huu, maeneo ya Kibona Lodge, washtakiwa Ngunyi na Dirangu wanadaiwa kuwapo nchini bila kuwa na kibali. Mshtakiwa Macha anadaiwa Julai 15, mwaka huu, kinyume cha sheria aliwahifadhi Ngunyi na Dirangu kuishi Tanzania wakati wakijua hawana kibali.

Katika mashtaka ya 11, inadaiwa kati ya Julai 20 na 26, mwaka huu, maeneo ya Kibona Lodge. Washtakiwa hao waliisababishia TCRA hasara ya Sh. 16,634,400.

Washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Ruboroga aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 20, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa wote wamerudishwa rumande kwa sababu mashtaka hayo hayana dhamana labda watakapoomba Mahakama Kuu.

# Uelewa kuhusu sheria waongezeka

**Na Happy Severine,** BARIADI

UELEWA wa wananchi juu ya masuala ya sheria mkoani Simiyu umeongezeka kwa asilimia 66 kutoka asilimia 10 mwaka 2016 kabla ya kuanza kwa mradi wa upatikanaji endelevu wa msaada wa kisheria.

Ofisa Ufuatiliaji na Tahimini wa shirika lisilo la kiserikali la KASODEFU, John Titus, alisema hayo jana mjini hapa alipozungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya Wakulima (Nanenane) yanayoendelea kufanyika viwanja vya Nyakabindi.

Titus alisema mwitikio wa wananchi juu ya masuala ya sheria umeongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na shirika hilo.

"Siyo siri kwa sasa uelewa wa jamii umeongezeka ukilinganisha na miaka ya nyuma kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi ya upatikanaji endelevu wa msaada wa kisheria mwaka 2016," alisema.

Titus alisema ongezeko hilo la uelewa limesaidia kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto pamoja na utoaji wa taarifa za matukio ya ukatili kwenye vyombo husika.

Aliongeza kuwa katika nane za maonyesho ya Nanenane wametoa elimu ya sheria kwa wananchi 1,900 na kati ya hao, 56 wanahitaji kusaidiwa huduma za kisheria. Naye Lila Masuke mkazi wa Wilaya ya Itilima, alisema kabla ya kutembelea banda la KASODEFU, hakuwahi kupata elimu ya sheria lakini kwa sasa anashukuru kwa kuipata elimu hiyo kwa kuwa itakuwa msaada kwake.

"Nimefurahishwa na elimu ya sheria inayotolewa katika banda la Legal Services Facility kwani imenipa mwanga wa kutetea haki zangu pale nitakapoona zinapokonywa," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika maonesho ya Nanenane kwa ajili ya kujifunza mambo mengi yakiwamo masuala ya kisheria, umiliki wa ardhi na mali zingine.

# Wasimamizi uchaguzi waonywa ushabiki siasa

**Na Tiganya Vincent,** NZEGA

MSIMAMIZI wa Uchaguzi wa Jimbo la Nzega Mjini, Philemon Magesa, amewataka wasimamizi wasaidizi ngazi ya kata kuepuka ushabaki wa kisiasa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi mkuu ujao kutoka kata 20 za halmashauri hiyo.

Magesa alisema ili wasimamizi wasaidizi wawe salama katika mchakato huo, ni vyema wakazingatia Katiba, sheria na kanuni zinasimamia uchaguzi.

Alisema hali hiyo itasaidia kuufanya uchaguzi kuwa mzuri, wenye ufanisi na kuondoa kabisa malalamiko au vurugu wakati wote wa mchakato.

Magesa pia alisema katika utekelezaji wa majukumu yao, ni muhimu wakavishirikisha vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi katika masuala ambayo wanastahili kushirikishwa.

Naye Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Glays Barthy, aliwataka walioteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambao ni wanachama wa vyama vya siasa, kuhakikisha wanajitoa katika vyama vyao ili kusimamia kazi hiyo kwa umakini.

Aliwataka wasimamizi wasaidizi hao kuwa makini na watu wa karibu nao kwa kujiepusha kutoa maoni ambayo yanaweza kusababisha uvunjifu wa sheria za uchaguzi na kanuni zake.

"Muwe makini na makundi mnayojihusisha nayo kwa kuepuka kutoa maoni ambayo yanaweza kusababisha kuonekana unashabikia upande fulani na kusababisha vurugu," alionya.

Alisema katika kipindi chote cha uchaguzi, wanapaswa kujizuia kujadiliana na makundi mbalimbali nyakati zote za shughuli za uchaguzi.

"Tunajua baadhi yenu mna kazi za vyama vya siasa. Baada ya kiapo hiki mnatakiwa kujitoa kabisa kuzungumzia mambo ya vyama vyenu ili kuwatendea haki wote. Wale wenye ushabiki wa ndani ni vyema wakauacha ili kutekeleza majukumu yao kwa mujibu Katiba, sheria na kanuni zinazosimamia uchaguzi," alisisitiza.

# Wasimamizi watakiwa kuheshimu sheria

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WASIMAMIZI wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Mtwara, wametakiwa kuheshimu sheria za uchaguzi na kanuni zake zilizowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)

Pia wamehimizwa kushirikisha vyama vya siasa na wadau wengine katika masuala ambayo wadau hao wanastahili kushirikishwa ili kuepuka hali ya kutoelewana itakayotokea katika uchaguzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Changwa Mkwazu, alisema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya siku tatu kwa wasimamizi wasaidizi hao yaliyofanyika katika ukumbi wa zamani wa halmashuri mjini hapa.

Alisema wasaidizi hao wa uchaguzi 68 ngazi ya kata wanapaswa kutambua kuwa wameaminiwa na kuthaminiwa na NEC, hivyo kupewa jukumu la kusimamia uchaguzi utakaofanyika Oktoba 28. Kutokana na hali hiyo, aliwataka wafuate kikamilifu sheria za uchaguzi.

Mkwazu alisema jukumu kubwa ambalo wanatakiwa kulifuata ni pamoja na kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni na sheria zilizowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. "Mnatakiwa kutambua kuwa mmeaminiwa na kuteuliwa kwa sababu mnao uwezo wa kufanya kazi hii. Mambo muhimu mnayotakiwa kuzingatia ni kujiamini na kujitambua na kwamba mnapaswa kuzingatia katiba ya nchi, sheria za uchaguzi na kanuni zake," alisema Mkwazu.

Alisema uchaguzi ni mchakato unaojumuhisha hatua na taratibu mbalimbali za kufuatwa na kuzingatiwa kwa kuwa ndizo msingi wa uchaguzi kuwa wa amani na utulivu.

Mkwazu alisema iwapo wasimamizi hao watafanya kazi kwa ufanisi, wataondoa malalamiko au vurugu wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuwapa uwelewa wa kutosha ili katika kutekeleza mchakato huo, wawe na elimu nzuri ya kufanikisha mchakato mzima wa uchaguzi.

# Aweso awatumbua mameneja maji kwa uzembe

**Na Francis Godwin,** IRINGA

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amemtumbua Meneja wa Maji Mkoa wa Iringa, Mhandisi Shaban Gelen pamoja na Meneja wa Maji Wilaya ya Mufindi, kutokana na uzembe wa ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi wa Sawala na Nyololo, wilayani humo.

Aweso alisema wakati Rais Dk. John Magufuli akiwaapisha baada ya kuwateua aliwaeleza mambo mawili likiwamo la kuwatumikia wananchi na wakishindwa atawatumbua.

"Kabla ya Rais hajanitumbua nawatumbua kwa kukwamisha utekelezaji wa miradi ya wananchi," alisema.

Aweso alisema, miradi hiyo ni ya muda mrefu na ahadi ya Rais ni kuona wananchi wanapata huduma ndani ya mwezi Agosti, mwaka huu, lakini watendaji hao kwa uzembe wamechelewesha pamoja na kupewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa tangi la maji ili wananchi wapate majisafi na salama.

Baada ya kukagua maendeleo ya miradi hiyo, alisema amefurahishwa nusu ya utekelezaji na anaona ni lazima kuchukua hatua ya haraka ya kuwapumzisha watendaji hao wakuu wa maji katika Mkoa wa Iringa na Wilaya ya Mufindi ili kuwapata watu watakaofanya kazi kulingana na matakwa ya serikali ya kuharakisha huduma hiyo kwa wananchi.

"Wananchi wetu wanahitaji kuona wanapata huduma ya maji na sio kupata maneno kutoka kwa watendaji wa serikali, wataalamu wamegeuka kuwa wanasiasa kwa kutoa maneno zaidi badala ya vitendo, hivyo nataka meneja wa maji mkoa wa Iringa atueleze lini mradi huu utakamilika," alisema Aweso.

Pamoja na kuwatumbua mameneja hao, Aweso alipongeza mradi wa maji wa Ilula kwa kutekelezwa vizuri na kuwatumia salamu mameneja wa maji wilaya na mikoa nchini kuwa katika ziara yake hiyo hatawafumbiwa macho na serikali haipo tayari kuadhibiwa na wananchi kwa kushindwa kutekeleza ahadi yake ya maji.

Meneja wa Maji Wilaya ya Mufindi, akizungumza kwa niaba ya Meneja wa Mkoa wa Iringa, Mhandisi Shabani pamoja na kuomba radhi wananchi kwa uzembe uliojitokeza, aliomba kupewa muda hadi mwezi ujao ili mradi wa Nyololo ukamilike.



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, akifungua mafunzo ya vijana 150 wa Jeshi la Akiba yaliyoandaliwa na wilaya hiyo, mkoani Pwani juzi, na kuendeshwa na Mshauri wa Jeshi la Akiba wilayani humo, Meja Mohamed Wawa (kushoto). **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Meneja TARURA asimamishwa kazi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mhandisi Victor Seff, ameagiza mkandarasi wa ujenzi barabara na madaraja Erasto Kwilasa wa mkoani Shinyanga, kutopewa kazi za ujenzi kutoka wakala huo kwa madai ya kutekeleza kazi chini ya kiwango.

Seff alibainisha hayo juzi alipofanya ziara katika Manispaa ya Shinyanga kukagua matengenezo ya madaraja ambayo yalisombwa na maji katika msimu wa mvua uliopita.

Alisema hajafurahishwa na utendaji kazi wa mkandarasi huyo kwa kujenga madaraja chini ya kiwango, huku mengine yakianza kuanguka hali ambayo ni hatari kwa watumiaji na kusababisha maafa makubwa.

"Nimepokea malalamiko mengi sana ya mkandarasi huyu juu ya utendaji wake wa kazi na nimekuja kujiridhisha mwenyewe. Ni marufuku kupewa kazi tena TARURA kwa sababu ukiangalia madaraja yote ambayo nimetembelea yamejengwa chini ya kiwango," alisema Seff.

Aidha, alisema ana msimamisha kazi Meneja wa TARURA Manispaa ya Shinyanga, Jolister Mtelani, kwa kushindwa kusimamia vizuri matengenezo ya madaraja, huku yakijengwa chini ya kiwango.

Kutokana na uamuzi huo, alisema nafasi yake itashikiliwa na Meneja wa TARURA wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, hadi atakapoletwa meneja mwingine. Pia alitoa angalizo kwa wahandisi kufanye kazi kwa ufanisi na kuacha kuwachekea makandarasi wazembe.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema alishamsweka ndani mkandarasi huyo kutokana na kufanya kazi chini ya kiwango na kubainisha alishamwonya meneja huyo wa TARURA manispaa kuacha kufanya kazi na makandarasi wasio na sifa.





Mratibu wa Mradi wa Elimu Jumuishi katika Kitengo cha Kanisa la FPCT, Jane Mgidange (katikati), akigawa vifaa vya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona, vikiwamo ndoo, sabuni na vitakasa mikono kwa mwanafunzi Shaff Juma mwenye ulemavu anayesoma darasa la pili katika Shule ya Msingi Nkuhungu, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TAMISEMI yaja kivingine huduma kwa wateja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imezindua kituo cha huduma kwa wateja ili kurahisisha utendaji kazi na kuwaepusha Watanzania kusafiri kwenda makao makuu ya ofisi hiyo kufuata huduma.

Wakati wa uzinduzi jana, Waziri wa Ofisi hiyo, Selemani Jafo, alisema kituo kimeanza kazi siku tatu zilizopita na wananchi 100 wamepata huduma.

"Kuanzisha kituo kipya cha huduma kwa wateja kitarahisisha wizara kutoa huduma zake na kufika kwa jamii kwa haraka. Niwaombe kuwaarifu Watanzania wote TAMISEMI imekuja na mfumo wa huduma kwa wateja. Tumieni mfumo huu wa huduma kwa wateja ambao TAMISEMI imeamua kuwaletea kwa ajili ya kupunguza watu kusafiri kuja makao makuu Dodoma kupata huduma," alisema.

Waziri Jafo aliwaomba wafanyakazi watakaokuwa wanahudumia wateja kufanya kazi yao kwa ufanisi bila kuchoka kwa kuwa wao ndio kioo cha wizara, huku wakizingatia kutoa huduma bora kwa mteja ili kupata mrejesho mzuri.

"Ninyi mna kazi kubwa sana ya kufanya kuliko mtu yeyote. Mwonekano wa kwanza una umuhimu, mwonekano wetu wa kwanza tukionekana vibaya, tutaonekana wabaya. Naomba mkajitume sana msichoke katika kazi yenu, lakini majibu yenu yanatakiwa yawe sahihi bila kuleta ubabaishaji wowote," alisema.

Alibainisha kuwa katika kituo hicho, wananchi watasikilizwa kwa urahisi na ukaribu zaidi.

"Lakini tutaongeza kasi kwenye kufanya kazi na kupata mrejesho kutoka kwa wateja wetu katika utoaji wa huduma," alisema. Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Mhandisi Joseph Nyamhanga, alisema kituo hicho kitakuwa mkombozi kwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kuwa itaongeza ufanisi na kupambana na rushwa kwa kundoa fursa ya wateja kukutana na watumishi. "Si kwa wateja wetu, hata kwa watumishi wetu maana TAMISEMI ina walimu ambao baadhi wanahitaji uhamisho na masuala mengine. Sasa badala ya kufunga safari kuja hapa watatumia kituo hiki. Nataka kituo hiki kitangazwe na kujulikana kwani kitakuwa mkombozi katika utendaji wa wizara," alisema. "Napokea simu nyingi sana za walimu kutoka kila kona na simu za wananchi kuulizia masuala mbalimbali na si rahisi kutoa majibu ya haraka hivyo naamini hata simu zinazopigwa kwangu na wasaidizi wangu zitapungua," aliongeza.

Nyamhanga alisema pamoja na kuwa ofisi yake imejitahidi kudhibiti utapeli, bado changamoto hiyo ipo na kuwa kituo hicho kutapunguza vitendo vya rushwa. Naye Msimamizi wa Kituo hicho, Antelma Mtemahanji, alisema kupitia mfumo huo, mteja atapiga simu na kueleza suala lake ambalo majibu yake yatatolewa papo kwa hapo kwa jambo ambalo halihitaji ufuatiliaji.

Alitumia fursa hiyo kuwasihi wakuu wa idara kutoa ushirikano wa karibu katika kujibu hoja za wateja wao kwa haraka na kuwa na majibu sahihi.

# Awataka wabeba mizigo kujisajili

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wabeba mizigo wa soko jipya la kisasa la Job Ndugai kujisajili na kuunda umoja ili kutambuliwa na wateja wao wanaowahudumia.

Yuna alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na wabeba mizigo hao.

Alisema hatua hiyo itawaepusha na uvamizi wa watu wengine wasio waaminifu kwa mizigo ya wateja, hivyo ni muhimu wakafanya hivyo ili wateja wawe na imani kwa upande wao. "Hili ni soko la kimataifa tena la kisasa, sasa linatakiwa kuendeshwa kwa mfumo wa kisasa na ninyi pia mnatakiwa kuwa na mavazi ambayo yatakayoonyesha nembo na namba ili pale itakapotokea mteja amepotelewa na mzigo, iwe nafuu kutambuana aliyefanya tukio hilo," alisema.

Ofisa huyo aliwataka kufanya kazi zao kwa malengo ya kujiongezea kipato badala ya kufanya kwa mazoea ambayo yamekuwa hayawaletei maendeleo zaidi ya umaskini miongoni mwao. Alisema kazi wanazozifanya sawasawa na zingine zinazofanywa hivyo wanatakiwa kujitambua ili kupitia mafanikio kupitia ubebaji wa hiyo mizigo.

"Wengi wenu hapa kipato chenu mnachopata kinaishia kwenye matumizi ya anasa kama vile unywaji wa pombe, hali ambayo inayowafanya kuonekana mnafanya kwa mazoea haina mafanikio kwenu hata kama kipato chenu ni kinaridhisha," alisema.

Mmoja wa wabeba mizigo, Jafeth Mazengo, alisema kuna umuhimu wa kusajili kwa kuwa itarahisisha kutambua hata kwa wale wasiokuwa waaminifu kwa wateja wanaowahudumia.

# CWT yaomba serikali kusaidia mradi wa mafunzo kwa walimu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimeomba serikali ikiunge mkono chama hicho katika mradi wake wa mafunzo ya walimu shuleni (SITT), unaolenga kuongeza mbinu rahisi za ufundishaji na ujifunzaji. Mradi wa SITT unaelekeza walimu katika shule za msingi kutumia zana rahisi zinazopatikana katika mazingira husika kwa ajili ya kujifunzia kwa vitendo, njia ambayo ni rafiki na humwezesha mwanafunzi kuelewa haraka.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mkuu wa Chama hicho, Deus Seif, alisema kama serikali itauwanga mkono, kuna uwezekano wa kuwafikia walimu katika mikoa yote sita ambayo mradi unatekelezwa kwa sasa na kuonyesha matokeo chanya katika sekta ya elimu.


"Tunaishukuru serikali kwa kuruhusu walimu kwenda kwenye mafunzo, lakini bado tunaiomba ituunge mkono maana tukisema tukae meza moja tukasema CWT bajeti yetu hii hapa, bajeti ya mfadhili hii hapa na serikali nayo ikasema na sisi tunaweka mkono, kutoka mikoa mitatu ikawa sita, huende ikawa mikoa 12 na baadaye kufikia walimu mikoa yote," alisema Seif.

Mratibu wa Mradi huo kutoka CWT, Donatian Marusu, alisema mradi huo umeanza mwaka 2000 kwa majaribio na utekelezaji wake rasmi ulianza mwaka 2012 na hadi sasa walimu 10,000 katika wilaya 21 za mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara wamefikiwa. "Hatua hiyo ni kwa awamu mbili, sasa tupo katika awamu ya tatu ya mradi katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Shinyanga na tumelenga kuwafikia walimu 3,000 katika mikoa hiyo kuanzia mwaka jana hadi mwakani," alisema Marusu.

Marusu pia alisema mradi huo unatoa mafunzo kwa walimu wa vyuo vya ualimu na kwamba Januari, mwaka huu, wataalamu kutoka Afrika Kusini walitoa mafunzo kwa wakufunzi na wakuu wa vyuo vya ualimu 24 katika vyuo sita.

Naye Mkuu wa Idara ya Elimu (CWT), Stella Kiyabo, alisema mradi huo umejikita katika kuboresha mbinu za kufundishia na kuzifanya ziwe rahisi hata kwa masomo yanayodhaniwa kuwa magumu. "Wakati mwingine baadhi ya masomo yanaonekana kama ni magumu kumbe ni kutokana na mbinu zinazotumika zinakuwa siyo rafiki kwa mwanafunzi," alisema Kiyabo.

Mwezeshaji wa Mafunzo hayo, Mwalimu Dawite Sagday, alisema mradi unatoa fursa kwa walimu wanaopata mafunzo pia kufundisha walimu wenzao, hivyo kupanua wigo kwa wale ambao hawajapata mafunzo hayo ambapo baada ya mafunzo walimu wanapaswa kutumia zana zaidi kuliko maneno.





# Shein ataka kipaumbele katika utafiti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameitaka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuweka kipaumbele katika kufanya utafiti unaohusiana na sekta za wizara hiyo kwa kuzingatia mazingira halisi na mahitaji ya wananchi na matukio mbalimbali ikiwamo milipuko ya maradhi ya mazao na mifugo.

Akizungumza juzi baada ya kufungua maonyesho ya wakulima (Nanenane), Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba, alisema kupitia utafiti huo wizara itapata taaluma na utaalamu mpya.

Dk. Shein alisema yanapotokea maradhi ya mifugo au mazao, wizara haipaswi kuishia kupiga dawa pekee, bali inatakiwa kutafuta chanzo cha maradhi hayo, kubuni njia za kuyaondoa na kuonyesha njia ili yasitokee tena.

Alisema katika siku za hivi karibuni, wakulima wengi wamejikita katika kilimo cha mazao mbalimbali ya biashara ikiwamo matikitiki, tungule (nyanya), matango na viazi vitamu, kupitia matumizi ya mbolea za kemikali.

Pamoja na uzuri wa kuendeleza kilimo, alisema kuna haja ya kufanya uchunguzi wa kitaalamu juu ya faida na hasara za kilimo cha aina hiyo, hasa katika afya ya udongo, ardhi, mazingira na virutubishi katika mazao yanayotokana na kilimo hicho.

Aidha, alisema tangu asili, kisiwa cha Pemba kinasifika kwa kuwa na ardhi yenye rutuba nzuri, jambo linalosababisha kupatikana mavuno mazuri kupitia matumizi ya mbolea za asili (kilimo hai), hali ambayo hivi sasa imebadilika.

"Mimi naamini kilimo hai kwa kutumia mbolea za asili bado kuna umuhimu mkubwa ndani ya jamii yetu. Hata hivyo, suala la kukiendeleza na upatikanaji wa masoko ya mazao yanayotokana na kilimo hicho linahitaji kufanyiwa utafiti," alisema.

Dk. Shein alisema watu wengi duniani wanaendelea kula vyakula vinavyotokana na kilimo hai kutokana na ladha ya asili ya vyakula hivyo pamoja na kuwapo uwezekano wa kupunguza athari za kemikali.

Alisema suala la utafiti huzijengea jina taasisi na nchi katika medani za kitaalamu duniani kwa kuzingatia mazao yatokanayo na kilimo hai kwa kuwa huuzwa kwa bei ya juu sana, ikilinganishwa na mazao yanayotumia mbolea za kemikali.

Pia aliitaka Wizara ya Wilimo kuwahamasisha wananchi juu ya uanzishaji wa mashamba ya viungo ikiwa ni hatua ya kuvutia watalii na kuwapatia wananchi kipato cha kuendesha maisha yao.

Alisema mashamba hayo yanaweza kuwa sehemu za huduma za vyakula vinavyotumia viungo hivyo, ambapo wageni wataweza kuona uhalisia wa matumizi yake.

"Mnaweza kuwahamasisha wananchi kuanzisha sehemu za maonyesho ya wanyama wetu wa asili zitakazokuwa vivutio muhimu kwa wazee na watoto hasa siku za sikukuu, kuna baadhi ya wanyama kama kima na tumbili wanaweza kuwa kivutio kikubwa kwa watalii na wananchi," alisema.

Alisema serikali imejipangia mikakati maalum kwa lengo la kuongeza uzalishaji kupitia mbinu bora, teknolojia ya kisasa, ujenzi wa miundombinu, utoaji wa thamani na upatikanaji wa masoko, pamoja na mitaji na uhifadhi wa chakula, ili kuongeza tija, kukuza uchumi na kuondoa umaskini.



Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar, Maryam Juma Sadala (Mabodi), akitoa maelezo ya kitaalamu wakati wa ufunguzi wa maonyesho ya wakulima Nanenane, katika viwanja vya Chamanangwe, Wilaya ya Micheweni Pemba juzi. **PICHA: IKULU**

# Aagiza maji kupelekwa mradi ujenzi makazi Makamu wa Rais

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAHANDISI wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) wanaosimamia usambazaji wa huduma ya majisafi na salama katika Mtaa wa Pagali, Chakechake kisiwani Pemba, wameagizwa kuandika maombi ya upatikanaji wa vifaa vilivyopungua ili mradi huo umalizike kwa wakati uliopangwa.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa nyumba ya makazi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Pagali kisiwani Pemba.

Balozi Iddi alisema itapendeza vifaa vinavyotumika katika mradi huo vinakuwa katika kiwango cha ubora unaokubalika ambavyo vitadumu kwa kipindi kirefu kinachosaidia kupunguza gharama kubwa za matengenezo ya mara kwa mara.

Alisema iko tabia mbaya na ya muda mrefu katika miradi mingi ya huduma za majisafi na salama inayotumiwa na baadhi ya wahandisi wanapopewa jukumu la kusimamia kazi huamua kununua vifaa vilivyo chini ya kiwango na matokeo yake miradi husika hufanya kazi muda mfupi na baadaye kuleta usumbufu kwa wananchi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA), Mhandisi Ramadhan Mussa Bakari, alisema wajenzi wa mradi huo kwa sasa wanasubiri kukamilika kwa uwekaji wa miundombinu ili wakamilishe kazi ndogo ndogo zilizobakia ikiwamo upakaji rangi. Mkurugenzi huyo alisema matengenezo yaliyobakia katika kipindi hiki yanatarajiwa kukamilika ndani ya mwezi mmoja na makabidhiano yanatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu au mwanzoni mwa mwezi ujao.

Alisema kinachozingatiwa ni namna ya kuwapata washauri na wataalamu wa masuala ya miti na bustani kutoka Taasisi ya Misitu na Manispaa ili bustani itakayooteshwa ilingane na hadhi ya nyumba za viongozi wakuu wa serikali.

# UVCCM Z'bar wamvaa Lissu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Zanzibar umemtaka mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kuacha kuwapotosha wananchi ili kujipatia umaarufu.

Kauli hiyo ya UVCCM imetolewa kutokana na madai ya Lissu kuwa mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Mwinyi, amechaguliwa bila ya ridhaa ya Wazanzibari.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Zanzibar, Mussa Haji Mussa, alimtaka Lissu na marafiki zake waache kuwadanganya Watanzania ambao wanafahamu kwamba CCM ndicho chama pekee kinachofuata utaratibu unaofahamika wa kupata viongozi wake kwa njia za kidemokrasia.

Mussa alisema Dk. Mwinyi alifuata utaratibu wa mchakato wa kupata viongozi na kuchaguliwa kuanzia uchukuaji fomu za urais kwa kuwahusisha wagombea 32.

Aidha, alisema wagombea waliochukua fomu wote walikamilisha masharti yaliyowekwa na chama ikiwamo kupata wadhamini katika mikoa ya Unguja na Pemba.

Pia alisema wagombea hao walijadiliwa katika vikao halali ikiwamo Kamati Maalumu ya Halmshauri Kuu ya CCM Zanzibar na baadaye walijadiliwa na kupigiwa kura katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM chenye wajumbe kutoka Zanzibar na Tanzania Bara.

"Huo ndio mchakato wa CCM katika kumpata mgombea wa urais wa Zanzibar ambao ulifuatwa na kutekelezwa na wagombea wote waliochukuwa fomu. Mshindi aliyeibuka na kupeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi mkuu alipata ridhaa zote ikiwamo kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM wenye wajumbe kutoka ngazi mbalimbali kuanzia wilaya," alisema.

Haji alisema katika kuonyesha mgombea wa urais wa Zanzibar ni chaguo la Wazanzibari, alisema alipowasili Unguja alipata mapokezi ya kihistoria yaliyovunja rekodi na kuwashirikisha wanachama na wafuasi pamoja na wananchi wa kawaida.



TEKNO TARATIBU Uk 14
WASIJE WAKAKUSIKIA

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI
TELE

JUMAMOSI AGOSTI 8, 2020



INSHALLAH!!

# Wema amshtakia Mungu

STAA wa filamu nchini, Wema Sepetu, ameshtaki kwa Mungu, akisema yeye ndiye anayejua jinsi gani anakabiliana na maneno makali yanayomchoma moyo.

Akizungumza hivi karibuni, Wema amesema bado kuna baadhi ya watu wanamsakama kwa kumuita majina ya kuudhi kutokana na kutofanikiwa kupata mtoto hadi sasa.

Hata hivyo, ameeleza pamoja na kuwa na kiu kubwa ya kupata mtoto wake, lakini hawezi kupingana na maamuzi ya Mungu ambaye ndiye anajua wakati wa kumpatia kile anachotamani.

Hata hivyo, ameeleza bado ataendelea kuomba na hata akiondoka duniani bado itamuuma akiwa amelala kaburini.

"Linapokuja suala la mtoto, nahisi kiu yangu itaisha pale nitakapomshika wa kwangu na itaendelea kuniuma mpaka nitakapopata wangu, itaniuma mpaka kesho hadi kifo na kama Mungu amenijalia nisipate sawa hamna shida, nitaingia kaburini bila mtoto bado nitaumia," Wema Sepetu.

Akizungumza suala la watu kuendelea kumsema kutokana na suala hilo, ameeleza hana la kuwajibu badala yake anamshtakia Mungu kwani yote ni mipango yake.

"Siwezi kuwajibu watu wanaoendelea kunisema vibaya, yote yataisha kwani wakati wa Mungu ni wakati sahihi, naamini atasikia kilio changu cha muda mrefu," amesema Wema.

Hata hivyo, amesema hawezi kuweka wazi uhusiano wake kwa sasa kwa sababu muda wa kufanya hivyo haujafika.

Amekiri kuwa ndani ya uhusiano na mwanaume ambaye hakumtaja na kuwaomba mashabiki wake kusubiri muda ambao atakuwa tayari kumtambulisha.

**BASI SAWA**

## Madee ungesema hayo mwanzo



KUFUATIA tukio la mwanamuziki wa Bongo Fleva, Mr Blue, kudondoka jukwaani kwenye tamasha moja wiki iliyopita, Madee amejitokeza na kushauri wasanii kuwa na bima za afya zao.

Madee amesema kuwa na bima za maisha na afya ni jambo la maana, kuliko kukimbilia kukata bima za magari kwa kuhofia kukamatwa na polisi.

"Nimeona video Herry Samir Mr blue ameanguka jukwaani, natoa pole kwa niaba ya wanamuziki wote, Mungu akusimamie urudi tena kazini. Ifike muda sasa wasanii mjikatie bima za maisha yenu, msikimbilie kukatia bima magari kisa unaogopa kukamatwa na traffic," ameandika kupitia ukurasa wake wa Twitter.

## Mama Nandy kawachosha wengi



BAADA ya mama mzazi wa msanii Nandy, Maria Charles Mfinanga, kusema kinaga ubaga kwamba ndoa ya binti yake na rapa Billnass ni kama ya kufikirika, mashabiki wa wasanii hao wamegubikwa simanzi.

Mashabiki wengi walitarajia kuona Nandy na Billnass wanafunga ndoa hivi karibuni, lakini kutokana kauli ya mzazi huyo, ndoto hiyo kama imeyeyuka.

"Tulitarajia kuona Billnass na Nandy wanakuwa mke na mume hivi karibuni, tumechoshwa na kauli ya mama wa Nandy ambaye anaonekana dhahiri hayupo tayari na jambo hilo," alisema Hamisi Hamad, wakati akichangia mjadala katika mtandao wa kijamii.

Akizungumza na EATV, Mama Nandy amesema "Bado wote ni watafutaji, wasogee kwanza kutimiza malengo kisha waingie kwenye ndoa, ndoa ipo tofauti siyo kama unafanya vitu vyako mwenyewe, wapo pamoja na washirikiana kwa vitu vingi hivyo wakae wajipange."

## Ali Kiba unaifahamu 'sapraizi' ya JPM?



MWIMBAJI nyota wa Bongofleva Ali Kiba, ameamua kutoa siri baada ya kusema siku ya mchezo wa "Team Kiba Vs Team Samatta" utakaofanyika kesho Uwanja wa Benjamin William Mkapa, Rais John Magufuli, atafanya 'surprise' ya nguvu.

Alikiba amesema Rais Magufuli amewaomba Watanzania kuendelea kutunza amani kwa sababu yaliyofanyika ni mengi wanachosubiri kuona matokeo.

"Nilimwomba Rais Magufuli aweze kutusaidia kitu kwa hiyo kuna uwezekano wa kuwa na surprise, msije mkashangaa Rais akaja kwa sababu yeye ni mpenzi wa burudani na anatukubali wote mimi pamoja na Samatta," amesema Alikiba.



# Lulu Diva kwa ndinga hili, piga makofi

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva anayefanya vizuri, Lulu Diva, ameamua kuonyesha ubabe wake baada ya kuonekana mitaani akiwa ndani ya gari la kifahari aina ya Jeep.

Lulu Diva anayejiita kama "The Boss Baby" amesema gari hilo si la kitoto kwani thamani yake ni shilingi milioni 300 na halifanani na masanii yoyote hapa nchini.

Gari hilo sasa linampa nafasi ya kuwa msanii wa kwanza wa kike anayemiliki gari lenye thamani kubwa.



# Snura hakuna shari isiyo na kheri

BIFU kati ya wanamuziki wa Bongo Fleva, Shilole na Snura, linazidi kupamba moto baada ya kila mmoja kuendelea kutupa madongo ya mbali.

Hivi karibuni Shilole alimshambulia Snura katika Tamasha la Girl Power, akimtuhumu kufurahia tukio la yeye kupigwa na Uchebe, jambo ambalo limemkera sana.

Hata hivyo, Snura amesema ameumizwa sana na tukio hilo, lakini yeye anamwachia Mungu na kushukuru kwa kile kilichotokea.

"Nimekaa kimya na kumwachia Mungu, maana itakuwa kama nongwa kuliendeleza ikiwa kama watoto wa kike kuongea masuala ya ugomvi muda wote, sina kinyongo na mtu yeyote kilichotokea ni changamoto katika maisha, namuachia Mungu maana hakuna shari isiyo na kheri," amesema Snura.

## Watoto wa Mitaani: Mazoea siku zote huzaa upofu

**Na Adam Fungamwango**

MAZOEA siku zote yana tabu. Haijalishi umezoea tabu au raha. Wapo watu ambao wamezoea kukaa kijijini, wanapofika mijini na kukaa wiki moja tu hamu inawaishia wanataka kurudi walikotoka. Ni kwa sababu ya mazoea.

Kuna wanaotoka mjini kwenda kijijini, nao wanapokutana na mazingira ya huko, yanawashinda kutokana na kuzoea kuishi mjini, hivyo wanashindwa.

Hata leo hii, mkazi wa Oysterbay anaweza kabisa kushindwa kuishi Manzese, na mkazi wa Manzese, akawa hawezi kabisa kuishi Masaki. Ni kwa sababu ya mazoea.

Hebu tuiangalie filamu hii inayoitwa 'Watoto wa Mitaani' ambayo ina funzo kubwa jinsi binadamu anavyoathiriwa na mazoea.

Imechezwa na wasanii wengi chipukizi, lakini wakiongozwa na Ben Blanco. Wengine ni Salma Juma, Peter Phimar, Kisegese, Kadogo, Dulla Said, Dogo Mandal, Julius Fred na wengineo wengi.

Ben na ndugu yake Peter wanakaa kikao na kukubaliana kuanzisha kituo cha kulelea watoto yatima. Baada ya kupata kibali kutoka serikalini, kazi inaanza ya kukusanya watoto mitaani.

Haikuwa kazi rahisi, Ben Blanco alikumbana na changamoto nyingi kutoka kwa watoto hao kuanzia wa miaka mitatu hadi 17, ambao wengi walikuwa wameshazoea maisha ya kuzurura, kulala jalalani na kula chochote kinachopatikana. Ni maisha ambayo wamezoea, hivyo kwenda kukaa kwenye kituo ilikuwa mtihani mkubwa.

Kwa tabu, Blanco anafanikiwa kuwashawishi baadhi ya watoto yatima, wa kike na wa kiume kujiunga na 'senta' yao.

Maisha yao yalianza kubadilika. Walianza kuwa wasafi kwa sababu ya kuoga mara kwa mara. Siha yao ilianza kubadilika, kwani walianza kunawiri. Ni kwa sababu walianza kula wanachokitaka na si wanachokipata. Pia walianza kusomeshwa. Hata hivyo bado baadhi ya watoto waliona hiyo ni kama kunyimwa uhuru wao.

Walizoea kuzurura kutwa nzima wakitafuta wasichokijua wala kuwa na uhakika wa kukipata. Lakini walizoea maisha hayo, hivyo maisha ya kuchungwa, kukaa kutwa nzima wakisoma tu, wakila, kunywa kiulaini, kufanya kazi mbalimbali za kituo, waliona kama ni aina fulani ya utumwa.





# Waliovuruga Msondo, Sikinde

**Na Adam Fungamwango**

HAPA Tanzania bendi hasimu ni Msondo Music Band na Mliamani Park Orchestra, hilo halina ubishi. Upinzani huu ulitokana na kuundwa kwa Mlimani Park Orchestra mwaka 1978 na kumtwaa Muhidni Maalim Gurumo kutoka Msondo.

Kama vile haitoshi mwaka mmoja baadaye wakamchukua mwimbaji tegemeo, Hassan Rehani Bitchuka na kuleta tafrani kubwa kwenye bendi hiyo.

Hapa ndipo upinzani wa bendi hizi ulipoanza na kuwa mahasimu wakubwa hadi leo hii. Sikinde mara nyingi ndiyo ilikuwa ina tabia ya kuchukua wanamuziki wa Msondo na hii ilizidi kuendelea uhasimu baina ya bendi hizo.

Kuna wanamuziki wengi waimbaji na wapiga ala, wametoka na kuingia kwenye bendi hizi mbili. Leo tunawaletea wanamuziki wapiga ala ambao wamewahi kuzipigia bendi zote mbili Msondo na Sikinde.

**SULEIMAN MWANYIRO -BASS GITAA**

Ukiacha waimbaji, Gurumo na Bitchuka, ambao ni waimbaji, mpiga gitaa wa kwanza ambaye kuchukuliwa na Sikinde kutoka Msondo ni Suleiman Mwanyiro.

Huyu aliondoka Msondo pamoja na Bitchuka kwenda Sikinde mwaka 1979. Kitendo chake cha kutoka tu Msondo kwenda Sikinde, tayari anekuwa ni mwanamuziki aliyepigia bendi zote mbili.

Kama vile haitoshi, Mwanyiro mpiga gitaa zito la bass, alirejea tena Msondo miaka ya '90, lakini kwa mara nyingine tena alihama na kwenda Sikinde na kukaa hadi alipofariki dunia 2004.

**KASSIM MPONDA - SOLO GITAA**

Ni mmoja wa wapiga magitaa ya solo mahiri kuwahi kutokea nchini Tanzania. Mponda alijiunga na Msondo mwanzoni mwa miaka ya '80. Na alikuwa mmoja wa wanamuziki waliodumu kwa muda mrefu kwenye bendi hiyo na kupiga nyimbo nyingi zinazotamba hadi leo, alipohama mwaka 1987 kwenda Sikinde, ingawa mauti yalimfika akiwa tayari ameshaanzisha bendi yake.

Naye akawa mmoja wa wanamuziki wapiga magitaa waliozipigia bendi zote mbili hasimu.

**URUKA UVURUGE - SOLO, RHYTHM**

Huyu ni mpiga magitaa mawili ya solo na rhythm, akitokea kwenye ukoo wa wanamuziki wa Uvuruge akiwa na ndugu zake, Maneno Uvuruge, Khalfan Uvurugena Fadhili Uvuruge.

Awali alikuwa Sikinde, wakati huo ndugu yake Maneno akiwa Msondo. Hata hivyo, baada ya ndugu yake Maneno kuondoka na kwenda bendi nyingine, Msondo walimchukua Uruka ili asaidie upande wa rhythm na wakati mwingine akipiga solo baadhi ya nyimbo, hivyo kuwa mmoja wa wapiga magitaa waliopitia bendi zote mbili.

**MOHAMED IDD 'CONTROL'- SOLO GITAA**

Ni mpiga gitaa la solo ambaye awali alikuwa Sikinde. Ni mmoja wanamuziki ambaye hakutegemewa kama ana weza kutoka Sikinde na kwenda Msondo.

Maisha yanabadilika. Miaka ya '90, Mohamed Idd 'Control', alijiunga na Msondo na wimbo wake unaomtambulisha sana ni 'Gloria' ambao alipiga solo na umahiri mkubwa, ingawa hakukaa sana kwenye bendi hiyo, akahama kabla ya kufikwa ya umauti.

**JUMA TOWN-SAXOPHONE**

Huyu ni mmoja wa wapuliza upepo mahiri nchini. Juma Town alikuwa mmoja wa wanamuziki wa mwanzo kabisa kutoka Msondo kwenda Sikinde, akitoka pamoja na kina Mwanyiro na Bitchuka mwaka 1979. Wengi wanamfahamu tu wakati yuko Sikinde, lakini ni wachache wanaofahamu kuwa awali alikuwa Msondo na kuondoka kwenye wimbi la Sikinde kukomba wanamuziki wa Msondo.

# Tekno taratibu wasije wakakusikia



MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Tekno Miles, amesema vitendo vya rushwa vinasababisha nchi hiyo kurudu nyuma kimaendeleo.

Akitumia akaunti yake ya Twitter, Tekno amesema baadhi ya viongozi wa juu wanaiba pesa kutoka hazina ya nchi hiyo na kuwasababishia wananchi kuwa na maisha magumu.

"Wewe kama kiongozi wa nchi unawaongoza watu na huwezi kuwapa hata kidogo, Mungu atakuadhibu katika njia zako za kutafuta pesa feki," ameandika.



## Flavour ndoa ya siri inanoga eti!

TAARIFA zinaeleza kwamba mwanamuziki wa Nigeria, Flavour, amefunga ndoa na mpenzi wake wa zamani Sandra Okagbue.

Kulingana na mtandao mmoja, mkali huyo wa muziki ambaye jina lake halisi, Blossom Martins, na Okagbue, wamefunga ndoa ya siri katika mji wa Onitsha Jumatatu.

Katika harusi hiyo, watu wachache walihudhuria na hakuna mtu aliyetakiwa kuingia na simu ya mkononi ili kuepusha kuvuja.

## Victoria waambie ukweli, wanawaumiza wenzao

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Victoria Inyama, amewataka wanawake kuwa na hofu na nguo wanazovaa watoto wao kuwaepusha na ubakaji.

Akizungumza baada ya kushiriki video moja katika ukurasa wake wa Instagram, amesema licha ya serikali ya Nigeria kuweka adhabu kali kwa wabakaji, lakini wazazi lazima kutoa tahadhari kwa binti zao kutovaa nguzo zinazoonyesha sehemu kubwa ya maungo yao.

"Ni hakika serikali haina uhakika wa kuweka adhabu itayozuia ubakaji, lakini kwa binti zangu tafadharini mavazi yenu msiyapunguze kiasi cha kuongeza ushawishi," amesema.





## Ace Hood imekuaje tena jamani?

RAPA kutoka Marekani, Ace Hood, kwa mara nyingine amemuita msanii mwenzake wa Ghana, Sarkodie, kuwa ni muongo.

Ace alimuita Sarkodie kuwa ana tabia ya uongo mwaka 2015, baada ya Mghana huyo kudai wimbo wa New Guy' ambao ameimba Ace kuwa ni wake.

Akiandika ujumbe kupitia Twitter, Ace Hood amesema "Ngoja niwaambini kuna uvumi wa uongo unaosambaa kuwa kufikisha kwangu wafuasi wengi ni feki, huo ni uongo," ameandika.

## Amkeni amkeni! Rihanna naye mama kijacho

MAMBO yanawaendea vizuri kati ya bosi wa lebo ya Mavin, Don Jazzy na mwanamuziki Rihanna, kutangaza wanatarajia kupata mtoto wao wa kwanza.

Don na Rihanna wote wakiwa wamejipatia umaarufu kutokana na kazi zao, wamekuwa 'kapo' inayovutia kwa sasa nchini Marekani.

Katika ukurasa wao wa Instagram, kila mmoja alitupia picha ikiwaonyesha wakiwa pamoja huku Rihanna akionekana tumbo limetokeza na kuashiria ni mjamzito.



MAKALA

# Viongozi wanaotokana na rushwa majanga kwa taifa

Na Dk. Enock Mlyuka

SERIKALI imekuwa ikisisitiza sana umuhimu wa utawala bora ili kufikia malengo ya taifa. Utawala bora ni jambo muhimu katika kukuza na kuimarisha amani, utulivu, ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

Katika kufanikisha azma hiyo, mkakati wa taifa katika mapambano dhidi ya rushwa, ni mwendelezo wa juhudi za serikali katika kuimarisha utawala bora. Hiyo ni kutokana na kutambua kuwa rushwa ni adui wa haki na maendeleo.

Wakati huu, Tanzania inaelekea katika uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Hii ni hatua muhimu katika utawala wa nchi kwani inakuza na kuimarisha demokrasia. Ni muhimu wananchi, vyama mbalimbali vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi wazingatie Katiba, sheria, kanuni na miongozo iliyopo katika uendeshaji wa uchaguzi.

Watu wamezoea vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi na wanaona ni jambo la kawaida unapowadia wakati kama huu. Wako wenye tabia ya kutoa vyakula, vinywaji, mavazi, fedha na ahadi zisizotekelezeka kwa nia ya kushawishi na kununua wapiga kura.

Maswali ya msingi ambayo kila mwananchi anapaswa kujiuliza ni je, viongozi wana uchungu na matatizo ya wananchi? Kwa nini wanasubiri hadi wakati wa uchaguzi ndipo wanakuja na ajenda za kusaidia wananchi? Kwa nini wema na uhusiano wa karibu na wananchi huonekana uchaguzi unapokaribia? Siku zote walikuwa wapi?




Watia nia wa CCM wakiwa wameshika maboksi ya kura zao. Vitendo vya rushwa vinaweza kusababisha kupatikana viongozi wasiofaa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) nchini Tanzania chini ya Kifungu cha (7) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007, imepewa jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa katika jamii ikiwamo rushwa katika uchaguzi.

Kutokana na majukumu hayo iliyopewa kisheria, ni imani kuwa TAKUKURU itatekeleza wajibu wake kwa weledi katika uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliopangwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Lengo la uchaguzi ni kupata viongozi bora na si bora viongozi. Mtu anayeomba ridhaa ya kuongoza toka kwa wananchi, apimwe kwa uadilifu wake na kazi alizofanya wakati uliopita. Mambo haya yanapaswa kuwa kigezo kikuu cha kupiga kura ya ndiyo au hapana.

Tanzania inahitaji viongozi wenye maono, watendaji, waadilifu, wazalendo, wanaochukia rushwa kwa dhati; wenye kuheshimu sheria na taratibu za nchi.

Sambamba na hayo, wanahitajika viongozi wenye roho ya kupenda umoja na mshikamano; kujali na kutanguliza mbele maslahi ya wananchi na taifa; wenye uchungu na rasilimali za nchi ili zisiporwe na walafi na mabeberu.

Viongozi wanaohitajika pia ni wale wenye kuguswa na matatizo ya wananchi na kutafuta njia za utatuzi wake kwa wakati; wenye nidhamu binafsi na wanaojua kujitawala; wabunifu, wakweli na wenye msimamo, wenye kusimamia haki; wenye juhudi na kujituma; wenye kupenda mabadiliko na kuondoa mazoea yasiyo na tija.

Tanzania ina njaa ya viongozi wanaoleta matokeo chanya katika jamii. Katika kipindi hiki kuelekea uchaguzi mkuu, wananchi wanapaswa kufahamu mahitaji hayo muhimu ya taifa kwa sasa.

Kwa mantiki hiyo, viongozi wasichaguliwe kishabiki kwani viongozi wanaochaguliwa kwa msingi huo hawana jipya zaidi ya kudumaza maendeleo na kuongeza umaskini kwa wananchi.

Uongozi unaoleta matokeo unahamasisha, unajali na kutia moyo wengine ili kuleta mabadiliko chanya yenye manufaa kwa mwananchi mmoja mmoja, jamii na taifa kwa ujumla. Hivyo, wananchi wajipange kutumia haki yao ya msingi ya kupiga kura na kuchagua viongozi bora wanaojua mahitaji ya jamii na taifa kwa wakati uliopo.

Aidha, wananchi wanapaswa kuepuka vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi. Kumchagua mtu kwa msingi wa rushwa ni kuporwa haki na wajibu wa kupiga kura kwa hiari. Wananchi wasiuze utu wao kwa kudanganywa na watu wenye uchu wa madaraka.

Mtu anayetoa rushwa ili achaguliwe kuwa kiongozi anadhihirisha tabia yake ya ubinafsi, uroho, tamaa na kutokuwa muadilifu. Ni kwa njia hii, wananchi wanapumbazwa kutokutumia haki yao ya msingi ya kupiga kura kwa hiari, hivyo kufanya upendeleo kwa wasiostahili. Matokeo yake jamii inapata viongozi vilaza, wajanja wajanja na wasio na msaada wowote kwa wananchi na taifa.

Kiongozi wa kweli anatoka kwa Mungu. Mungu anachagua kiongozi kupitia kura za watu, hivyo mtu anayetoa rushwa ili achaguliwe kuwa kiongozi anakuwa hajaitwa na Mungu kuwatumikia wananchi, bali amejiita mwenyewe katika uongozi kwa kuununua.

Pia kiongozi anayetokana na rushwa kwa vyovyote vile nafasi yake ya uongozi itamtumikia yeye zaidi kuliko utumishi kwa wananchi. Viongozi wa aina hii ni majanga kwa taifa na wananchi, hivyo wananchi wanapaswa kuwaogopa kama kirusi cha corona.

Wananchi wanapochagua kiongozi wasiangalie haiba yake, kabila lake au dini yake. Mtu anapochaguliwa kuwa kiongozi, hachaguliwi kama mtu bali huchaguliwa kutokana na huduma yake na vipawa vyake vya uongozi.

Kwa msingi huo, ni muhimu wananchi kuwa makini wakati wa uchaguzi na wachague kwa busara. Wanapochagua viongozi wasiofaa, maana yake wamechagua kudumaa katika maendeleo na maisha.


Ustawi na maendeleo ya taifa hutegemea aina ya viongozi wanaochaguliwa kwani kila kitu hufanikiwa au kutokufanikiwa kutokana na uongozi. Hitaji la nchi kwa sasa ni viongozi makini, waadilifu, waaminifu, wawajibikaji, wenye uwezo wa kwenda na kasi ya mabadiliko iliyopo na wenye nia ya dhati ya kuwatumikia wananchi.

Watu hawatajali kiasi gani kiongozi anajua hadi wajue kiasi gani anajali, hivyo wananchi wajiandae kuchagua viongozi ambao watafahamu kwamba wamechaguliwa kuongoza kwa niaba na kwa ajili ya watu wote na kwamba wameitwa kutumika wakati huu ambao ni mgumu.



Kura za wanachama walioomba kugombea ubunge zikihesabiwa.

**■Mwandishi wa makala hii ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Mtafiti, Mshauri, Mwanataaluma katika Theolojia, Maadili na Uongozi wa Rasilimali Watu.**




# Corona ilivyodhihirisha umuhimu wa takwimu

Na Mwandishi Wetu

ILIKUWA taharuki kwa dunia nzima kutokana na taarifa za kuibuka kwa ugonjwa hatari wa homa ya mapafu (Covid-19) unaosababishwa na virusi vya corona.

Tangu kuanza kwa ugonjwa huo ambao uligharimu maisha ya maelfu ya watu, watu wamekuwa wakifuatilia kwa karibu habari au matangazo yanayotolewa na magazeti, luninga, redio za kimataifa na kitaifa.

Kutokana na ufuatiliaji huo, kumekuwa na kazi kubwa ya kutoa takwimu kuhusu maambukizi, vifo na waathirika wa ugonjwa huo tangu ulipotokea katika Jimbo la Wuhan, China, mwanzoni mwa mwaka huu. Mifano michache ni kama vile tangu Aprili 8, mwaka huu, waathirika wa ugonjwa huo duniani 1,487,870 na vifo 88,630.

Mataifa ambayo yalipata pigo kubwa wakati huo ni Italia, Marekani, Hispania na Uingereza. Nchini Marekani, waliripotiwa wagonjwa 432,438 na vifo 14,808 wakati Uingereza vifo vilikuwa 7,100. Afrika wagonjwa walikuwa zaidi ya 10,000 na vifo 520, huku nchi zilizoathirika sana zikiwa Kenya, Afrika Kusini na Nigeria.

Kwa kipindi hicho, wafanyakazi wengi walipunguzwa kazi. Marekani, kwa mfano, waliopunguzwa walikuwa kati ya milioni tano na milioni saba wengi wakiwa watu weusi na walatino.

Mashirika makubwa ya ndege kama vile Emirates, Qatar na British Airways zaidi ya wafanyakazi 20,000 walipunguzwa kutokana na ugonjwa huo. Uchumi wa Uganda ulizorota na mfumuko wa bei ulifikia asilimia 4.1 wakati Morocco uwekezaji uliporomoka kwa kiwango cha juu zaidi tangu mwaka 1995.

Vilevile, Mei 5, mwaka huu, vyombo vya habari vilitangaza kuwa Mei 2 kulikuwa na wagonjwa wa Covid-19 duniani wapatao 3,392,771 na vifo 241,194 na Mei 4 wagonjwa duniani walikuwa 3,534,544 na vifo 248,169. Tarehe hiyo hiyo, Marekeni iliripotiwa kuwa na wagonjwa 1,161,805 na vifo 67,798 tangu mwanzoni mwa mwaka huu.

Kwa takwimu za Julai 5, mwaka huu, maambukizi ya corona duniani yalikuwa 11,477,724 wakati vifo jumla vilikuwa 534,938. Afrika Kusini pekee iliripotiwa siku hiyo kuwa waathirika walikuwa 196,750 na vifo 3,199 tangu ugonjwa huo uibuke. Julai 11, kwa dunia nzima vifo iliyotangazwa vilikuwa 559,000 kati ya waatharika 12,400,000 huku Brazil ikiwa na waatharika 70,000.

Nchi zote, kutokana na tatizo hilo, zimekuwa na juhudi za kuchunguza ugonjwa wa Covid-19 kwa afya za watu wao na kuripoti maambukizi, waliopona na vifo, lakini athari zilizojitokeza kwenye uchumi.

Watu wa kada mbalimbali wamehusika na upatikanaji wa takwimu hizo wakiwamo wafanyakazi wa sekta ya afya, viwanda na biashara na kadhalika. Janga la COVID-19 limemulika umuhimu wa taaluma ya takwimu katika sekta mbalimbali ili kuwezesha mipango mahsusi ya kupambana na kutokomeza gonjwa hilo.

Utoaji huo wa tamwimu, umeonyesha umuhimu kwa taasisi zinazotoa mafunzo ya takwimu kujikita zaidi katika uelimishaji wa aina mbalimbali ikiwamo mafunzo ya muda mrefu na mfupi, elimu kwa mtandao na masafa ili kuhakikisha takwimu zinazotolewa zimefuata misingi ya kitaaluma.

Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) kilichoko Dar es Salaam, Dk. Frank Mkumbo, alibainisha kwamba ndicho kinachoandaa wataalamu wa takwimu rasmi kwa nchi za Afrika.

EASTC inachohudumia nchi wanachama 19 ambazo ni Tanzania, Kenya, Lesotho, Malawi, Somalia, Sudan, Swaziland, Tanzania, Uganda, Zambia, Zimbabwe, Afrika Kusini, Eritrea, Mauritius, Namibia, Shelisheli, Sudani Kusini na Gambia.

Pia alisema ni chuo pekee Afrika kinachofundisha takwimu rasmi kwa lugha ya Kiingereza, hivyo kufanya hata nchi zisizo wanachama kupeleka wanafunzi zikiwamo Nigeria, Liberia, Ghana na Rwanda.

Chuo hicho kilianzishwa mwaka 1965 kwa lengo la kutoa mafunzo ya takwimu rasmi kwa kufundisha kozi mbalimbali kwa mfumo wa utaalamu wa ustadi kuanzia astashahada (cheti) hadi shahada ya umahiri.

Kutokana na umuhimu wa takwimu kama ilivyojionyesha katika suala la corona, chuo hicho kimedhamiria kupanua wigo wa mafunzo katika nyanja mbalimbali za takwimu ikiwamo kilimo na uchumi, biashara, na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Kozi hizo, kwa mujibu wa Dk. Mkumbo, zitaongeza utaalamu katika ukusanyaji wa taarifa katika maeneo tajwa kwa kutumia mbinu za TEHAMA.

Tathmini ya mahitaji imeonyesha uhitaji mkubwa wa kozi hizi katika karne hii ili kuwezesha Tanzania kuvuka malengo ya kufikia kiwango cha juu cha daraja la uchumi wa kati.

Katika kushiriki kuboresha mifumo ya takwimu nchini, alisema chuo kimebuni mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za kiutawala ili kupata taarifa zinazoendana na wakati kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Ubunifu huo ni pamoja na mkakati wa kuhuisha rejesta ya wakazi katika mfumo wa kielektroniki kwa kushirikiana na Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) chini ya uratibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Lengo ni kuhakikisha serikali inapata takwimu bora ili kupanga mipango ya maendeleo.

Chuo pia kwa kushirikiana na NBS, kilishiriki katika kuandaa makadirio ya idadi ya watu kupitia Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 katika ngazi za kitongoji, kijiji, mtaa, kata, wilaya, mkoa hadi taifa kabla ya Uchaguzi wa Oktoba mwaka 2015.



Mwanafunzi akinawa mikono ikiwa hatua ya kujikinga na corona. Takwimu kuhusu maradhi ya ugonjwa huo na madhara yake, vilikuwa chachu ya watu kuchukua tahadhari. **PICHA: MTANDAO.**

Takwimu hizi ndizo zilizotumika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika kupanga mipango yote ya vifaa na idadi ya wapigakura. Huo ni mchango mkubwa ulifanywa na Chuo kwa kuwa takwimu hizi ndizo zilizotumika kupanga na kutekeleza matayarisho yote ya uchaguzi.

Pia, chuo kilishiriki katika kuandaa mifumo ya takwimu kwa ajili ya Tume ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (PCCB) na Jeshi la Polisi na sasa kinaandaa mifumo kama hiyo kwa ajili ya Bodi ya Kahawa Tanzania na Tume ya Vyama vya Ushirika, VICOBA na Wizara ya Sheria na Katiba.

Ili kutimiza azma ya kutoa takwimu bora na sahihi, chuo kimetoa mafunzo kwa taasisi mbalimbali zikiwamo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wizara ya Fedha na Mipango, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tanzania (VETA).

Aidha, katika kuhakikisha upatikanaji wa takwimu unakuwa bora na kutumiwa ipasavyo, chuo kimekuwa na ushirikiano na mashirika ya kimataifa zikiwamo Benki ya Dunia, Umoja wa Mataifa (UN), Shirika la Kilimo na Chakula (FAO) na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB).

Ni dhahiri kuwa pasipokuwa na takwimu zilizotafsiriwa vyema kulingana misingi, mbinu na vigezo mbalimbali vilivyowekwa katika ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji, maendeleo endelevu yatazorota.

Umuhimu wa takwimu kwa kiasi kikubwa unaonekana kupitia matumizi yake, kama ilivyodhihirika katika kipindi hiki cha COVID-19 kwa namna ilivyosaidia katika sekta ya afya.

Kutokana na ukweli huo, ni dhahiri kwamba takwimu ni muhimu katika kila sekta ili kuwezesha kutambua mahitaji ya jamii katika nyanja mbalimbali hata kuchukua tahadhari na kupima matokeo.

# Msumbiji yakana kuhusika mlipuko Lebanon

**MAPUTO, Msumbiji**

MAMLAKA ya Bandari nchini Msumbiji, imekanusha madai kwamba meli yake ilihusika kubeba mzigo uliosababisha mlipuko katika Bandari ya Beirut.

Kulingana na Shirika la habari la AFP, inadaiwa meli inayoitwa MV Rhosus ilitoka Bandari ya Beira, nchini Msumbiji, na ilisafiri hadi Lebanon na kushusha mzigo ambao ulihifadhiwa ndani ya ghala moja.

Hata hivyo, taarifa kutoka mamlaka hiyo ilisema haijui chochote kuhusu meli hiyo.

"Mamlaka ya bandari haijui meli ya MV Rhosus iliacha mzigo katika Bandari ya Beirut," ilieleza mamlaka hiyo.

Inasema hakukuwa na tangazo la kuwasili kwa meli bandarini hapo ndani ya siku saba mpaka 15.

Lakini maofisa wa bandari ambao hawakutaka majina yao yatajwe, waliiambia AFP kuwa ingawa meli hiyo iliwasili katika Bandari ya Beira, lakini safari yake ilikuwa haipaswi kuishia Msumbiji.

Ilidaiwa meli hiyo inawezekana ilibebeba shehena ya milipuko kwa ajili ya migodi katika nchi za Zambia na Zimbabwe.

Mamlaka inayofuatilia mienendo ya meli, ilisema kuwa meli moja inayopeperusha bendera ya Moldoval, iliwasili Beirut tangu Novemba 2 mwaka 2013 haijawaondoka.

Wakati huo huo, wafanyakazi wa uokoaji na askari kutoka Jeshi la Lebanon, wanaendelea na shughuli za uokozi kufuatia mlipuko mkubwa uliotokea kwenye Bandari ya Beirut.

Katika mlipuko huo ulisababisha vifo vya watu wasiopungua 149 na kujeruhi wengine zaidi ya 5000.

Katika eneo hilo la tukio, kumekuwa na shughuli nyingi huku matingatinga yakijaribu kuondoa vifusi katika jengo kulikotokea mlipuko huo.

Jengo hilo lilikuwa limehifadhi tani 2,750 ya kemikali ya ammonium nitrate.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Italia, Luigi Di Maio, ameahidi kuwa nchi yake itaisaidia Lebanon.

**BBC**



Mtayarishaji wa vipindi vya runinga nchini Lebanon, Tony Ahwaji, ambaye alijeruhiwa katika tukio la mlipuko bandarini, akiwa amekaa juu ya jengo kuangalia uharibifu uliotokana na tukio hilo. **(PICHA: AFP)**

# Mwanamfalme Saudi Arabia ashtakiwa kupanga mauaji

**WASHINGTON, Marekani**

KASHFA za kupanga mauaji bado zinamwandama mrithi wa kiti cha ufalme wa Saudi Arabia, Mohammed bin Salman, baada ya kushtumiwa kutaka kumuua aliyekuwa jasusi wa nchi hiyo.

Inadaiwa Bin Salman, alituma mamluki nchini Canada ili kumuua ofisa wa ujasusi wa Saudi Arabia, Saad al-Jabri, ambaye anaishi uhamishoni.

Hata hivyo, kulingana na nyaraka zilizowasilishwa katika mahakama moja nchini Marekani, zinadai mpango huo haukufanikiwa.

Mauaji hayo yalipangwa kufanyika siku chache baada ya kufanikiwa kuawa kwa mwanahabari Jamal Khashoggi, ndani ya jengo la ubalozi nchini Uturuki.

Ofisa huyo wa ujasusi alikimbilia uhamishoni miaka mitatu iliyopita. Tangu wakati huo amekuwa chini ya ulinzi binafsi.

Inasemekana mpango huo ulifeli baada ya maofisa wa uhamiaji wa Canada, kuanza kushuku kikosi hicho walipokuwa wanajaribu kuingia kupitia uwanja wa ndege wa kimataifa wa Toronto Pearson.

Kwa miaka mingi, Jabri, alikuwa kiungo muhimu katika huduma ya ujasusi ya siri Uingereza na mashirika mengine Magharibi.

Katika mashtaka hayo yenye kurasa 106, yaliyofunguliwa katika Mahakama ya Washington DC, yanamtuhumu mwanamfalme huyo kwa kujaribu kumuua Jabri ili kumnyamazisha.

Katika madai yake, Jabri alieleza analengwa kuuawa kwa sababu yeye anajua taarifa nyeti ikiwamo ufisadi na usimamizi wa kikundi cha mamluki nje ya nchi hiyo kilichopewa jina la kikosi cha Tiger.

Wafuasi wa kikundi cha Tiger, pia walihusika na mauaji ya Khashoggi, ndani ya ubalozi wa Saudi, mjini Istanbul 2018.

**BBC**

# Trump amshambulia Biden hadharani

**NEWYORK, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amemshambulia mpinzani wake kutoka Chama cha Democrat, Joe Biden, kuwa anakwenda kinyume na Mungu.

Hata hivyo, kiongozi huyo alitabiri uchaguzi wa mwaka huu utakuwa na mpambano mkali wa kisiasa.

Trump alitoa kauli hiyo wakati wa ziara yake katika Jimbo la Ohio, na alikuwa akijaribu kuongeza ushawishi wakati akielekea katika eneo muhimu la majimbo ya Midwestern ambako alipata uungwaji mkono katika uchaguzi wa mwaka 2016.

"Biden anampinga Mungu, anapinga bunduki," alisema Trump.

Biden, ambaye Mkristo kutoka dhehebu la Katoliki, anaongoza katika kura ya maoni na kuashiria Chama cha Democratic kitatoka kifua mbele.

Mgombea huyo ambaye aliyekuwa Makamu wa Rais wa Barack Obama, mara kadhaa alisikika akisema jinsi imani yake ilivyosaidia kukabiliana na vifo vya mke wake wa kwanza na binti yake katika ajali ya gari mwaka 1972.

ZO CHA PICHA,GETTY IMAGES

Awali akiwa Cleveland, Trump, alimwita Biden kama mtu anayefuata ajenda za wanasiasa wenye misimamo mikali wa mrengo wa kushoto.

"Ukidhuru Biblia unamdhuru mungu. Atamkasirisha Mungu kwa kufanya kampeni chafu za uchaguzi." Alisema Trump.

**BBC**

# Rais Quattara kuwania tena baada ya kukosa mrithi wake

**ABIDJAN, Ivory Coast**

RAIS wa Ivory-Coast, Alassane Ouattara, atangaza kuwania tena urais katika uchaguzi wa Oktoba mwaka huu.

Ouattara, alisema ameitikia wito wa wananchi waliotaka awanie nafasi hiyo kwa awamu nyingine.

Kinyang'anyiro cha urais kilichukua mwelekeo mwengine baada ya Waziri Mkuu Amadou Coulibaly, aliyeonekana kuwa chaguo la Ouattara kumrithi kufariki dunia kwa ugonjwa wa moyo mnamo mwezi uliopita.

Hata hivyo, uamuzi wake wa kujitosa kwenye kuwania nafasi hiyo, huenda ukaibua tuhuma za ukandamizaji wa demokrasia wakati wa mihula yake miwili uongozi.

Hapo awali, aliwahi kusisitiza kufanyike mabadiliko ya katiba ili kumwezesha kuwania muhula wa tatu madarakani.

**DW**

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

## Mauaji Harusini- 24

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

EDDY alikumbuka maneno aliyoongea na msichana yule aliyekutana naye wakati akijifanya kuelekea msalani, akaongea naye kwa sekunde kadhaa, kabla ya kuelekea msalani kupoteza lengo, haraka, akarejea kumuwahi Shani asile kile chakula ambacho alikuwa na wasiwasi nacho, baada ya awali kuokota kifuko cha sumu, kilichoanguka kutoka kwa mhudumu yule wa kiume wa hoteli hiyo ya ABC Club.

Akiwa kitandani, Eddy alikumbuka jinsi alivyotoka tena kuelekea msalani, akampa ishara mhudumu yule yule wa kike amfuate na kumpa maelekezo kadhaa.

"Unakiona kile chakula kilichopo pembeni?"

"Ndiyo."

"Shika hii." Eddy alimkabidhi mhudumu yule kibunda cha noti mpya shilingi laki moja.

Ingawa mhudumu yule hakujua idadi kamili ya pesa zile, lakini alijua ni pesa za kutoka, lakini alizipokea akiwa na mshangao.

"Ananitaka?" Aliwaza. "Lakini huyu si ana yule msichana pale?" Mawazo yalizidi kumvuruga mhudumu yule.

"Usijali dada mzuri, unaitwa nani?"

"Diana."

"Okay, Diana, naomba unifanyie kazi moja tu, lakini iwe siri yangu mimi na wewe, usimwambie mtu."

Diana alibaki amepigwa na butwaa asijue akatae au akubali, bila hata kujua ni kazi gani anayotaka kuambiwa.

"Ni hivi, nataka uje uchukue kile chakula kilichopo pembeni yetu, alicholeta yule mhudumu mwenzako wa kiume. Ukichukue, lakini usiende kukimwaga, ukiweke sehemu yoyote ile nzuri, ukihifadhi kwa sababu mimi nataka kukichukua." Eddy alimwambia Diana.

Bado kwenye uso wa mhudumu huyo ulionekana kama kuna maswali mengi ya aliyokuwa anajiuliza.

"Diana, tafuta mfuko, kimwage chakula hiki kwenye mfuko, halafu kama unaweza kutoka nacho, leo, kesho au kesho kutwa tuwasiliane, halafu unikabidhi, nakihitaji."

Mshangao wa Diana ulikuwa ni kwa nini mwanaume yule anakitaka kile chakula ambacho hakikuliwa na yeye au mpenzi wake. "Je, anataka kumpeleke mbwa?" Alijiuliza.

"Lakini kwa nini aseme asijue mtu? Kwani kama ni kumpelekea mbwa si angemwambia tu akakikuchukue, akatafute mfuko akifunge na kumpelekea, badala yake anataka iwe siri?" Bado Diana alijiuliza.




**Diana, tafuta mfuko, kimwage chakula hiki kwenye mfuko, halafu kama unaweza kutoka nacho, leo, kesho au kesho kutwa tuwasiliane, halafu unikabidhi, nakihitaji.**

Lakini kwa sababu tayari alikuwa na pesa mkononi. Na pia kwake haikuwa kazi kubwa sana. Ni kukichukua tu, kwenda jikoni kutafuta mfuko madhubuti na kukitia humo, baadaye kutoka nacho, basi alikubali.

Haraka, Walibadilishana namba za simu na kazi ikawa imekamilika.

Siku hiyo Eddy alitarajia kutaka kumpigia simu Diana ili wakutane sehemu akichukue chakula hicho.

Lengo ni kukipeleka kwa mkemia mkuu ili kujua kama kina dalili yoyote ya sumu. Na kama sumu ni ya aina gani? Kama haina basi wasiwasi wake utakuwa ni wa bure.

Lakini kama kuna sumu ndani ya chakula. Na yeye aliokota kifuko cha sumu kilichoangushwa na mhudumu aliyemletea Shani chakula, basi tatizo litaanzia hapo.

**********************************

Ndani ya mgahawa mmoja maeneo ya Mburahati jijini Dar es Salaam, kulikuwa na watu wengi waliokuwa wakiingia na kutoka kupata chakula cha mchana.

Ulikuwa ni mgahawa wa kawaida tu, ukitumiwa na watu wenye kipato cha chini na cha kati pia.

Kama kawaida Eddy alikuwa ameingia ndani ya mgahawa huo dakika 15 kabla ya mwenyeji wake.

Alikuwa ameaihidiana naye kumletea mzigo walioahidiana.

Hatimaye mgeni aliingia. Pamoja na kwamba alimuona kwa mara ya kwanza kwenye hoteli ya ABC Club, lakini Eddy alimtambua vema.

Pamoja na kwamba siku hiyo amependeza zaidi kuliko siku ile, lakini Eddy hakushindwa kumtambua.

Alipojidhihirisha kuwa mgeni wake hakuwa na mgeni mwingine alimwita. "Diana, karibu hapa."

Kwa madaha Diana alijisogeza kwa Eddy na kuketi kwa maringo. "Umependeza sana." Eddy alimchombeza.

"Ahsante."

"Kumbe zile sare zenu zinaficha vitu vizuri kama hivi."

Diana alianguka kicheko chepesi na kuinamisha kichwa chini.

"Agiza unachokitaka."

Diana aliagiza chips, kuku na soda baridi, huku Eddy alitaka aletewe ugali, nyama choma na maji baridi.

Walikula taratibu na kuongea mambo mengi ya msingi, mzaha na kimaisha.

Eddy hakutaka Diana ajue kila kitu kuhusu yeye kushuku jambo, badala yake alitaka ajue tu kuwa anahitaji mzigo ule tu alioagiza.

Ndiyo maana hakutaka hata kumwambia chochote kuhusu mhudumu mwenzake Fikiri.

"Huu hapa mzigo wako, vipi wenzetu una mbwa unawapelekea? Na kwa nini sasa ulitaka iwe siri?" Diana aliuliza swali ambalo Eddy alijua kuwa ataulizwa.

"Nia yangu ilikuwa ni vitu viwili kwa mpigo, kwa hiyo nikatengeneza mazingira ili nilipate kwa pamoja. Na kweli lao imekuwa hivyo." Eddy alijibu alimwangalia Diana kwa tabasamu jepesi.

Alionyesha mshangao. "Ulikuwa na nia gani?"

"Nilikuwa nataka chakula hiki kwa ajili ya mbwa wangu nyumbani, lakini pia nilikuhitaji wewe."

Diana hakushangaa kutakiwa na mwanaume mzuri, mtanashati aina ya Eddy, lakini alishangaa alipoambiwa akusanye chakula kile, halafu asijue mtu yoyote, akichukue, aende nacho nyumbani, halafu amletee hapo walipokutana.

"Ni hivi Diana, mimi nilipokuona tu siku ile nilikupenda sana, lakini nilikuwa na yule msichana mwingine, kwa hiyo sikuwa na uwezo wa kukwambia kuwa nakupenda. Kwanza ningeanzaje pale? Halafu ungekataa kwa sababu kulikuwa na mwanamke mwingine. Na kwa sababu nilikuwa nahitaji chakula kwa ajili ya mbwa wangu, niliagiza sahani tatu pale, halafu nikakwambia wewe ukichukue, ukitunze na ukiletee hapa," alisema maneno ambayo taratibu yalianza kumuingia Diana.

"Nia yangu namba moja ulikuwa ni wewe na umekuja, huo mzigo nao ni chakula cha mbwa wangu, kwa sababu ningekwambia uje mwenyewe tu, sidhani kama ungekubali."

"Mhh haya baba umeshinda." Diana alikubali, huku nyuma ya pazia kukiwa na siri kubwa.

Eddy aliamua kumridhisha Diana kwa sababu moja tu. Kutomfanya awe na wasiwasi na asijiulize maswali mengi kiasi cha kuongea kwa watu bila kujua, hasa wahudumu wenzake, kwa sababu yangemfikia Fikiri aliyeangusha kifuko hicho cha sumu.

*********************************************

"Nachohitaji ni kuangalia hiki chakula kama nina aina yoyote ile ya sumu. Na kama ni sumu basi ni ya aina gani. Basi ni hilo tu." Eddy alimtazama Mkemia Mkuu wa Serikali aliyekuwa ametuna kwenye ofisi yake.

Ilikuwa ni baada ya maongezi ya dakika kumi hivi, Eddy alipotoa kitambulisho na kujitambulisha kuwa ni Ofisa Usalama wa Taifa.

Denis Mataruma aliyekuwa ameshika nyadhifa hiyo miezi sita iliyopita, aliinua simu na kumwita mmoja wa wafanyakazi wake.

Alipofika alimtaka kuchukua mkoba aliokuja nao Eddy.

"Humo kuna chakula. Chakula chenyewe ni biriani ya kuku. Kinachotakiwa ni kukipeleka maabara na kutambua kama kuna chembechembe yoyote ile ya kitu kinachohisiwa kuwa ni sumu. Na kama itagundulika kuwa sumu, kinachotakiwa ni kujua ni sumu ya aina gani. Kama hakuna vile vile jibu linatakiwa." Bosi aliamuru na Eddy alipokewa mzigo huo.

"Vizuri Eddy, nadhani baada ya siku mbili kila kitu kitajulikana na ningependa uje wewe mwenyewe hapa hapa uchukue majibu."

"Na ndivyo itakavyokuwa." Alijibu.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


### KUPOTEA KWA CHETI



**Said Hemed Swalehe** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la Saba chenye namba **0549474** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2018, na cheti cha kuzaliwa. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **PWA/MLA/RB/91708/2020**

115849702

### KUPOTEA KWA KADI

**EMMANUEL NGEREJA NKWIWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **MITSUBISH FUSO FIGHTER** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 271 DQL** YENYE CHASSIS NO **FK417H540280** NA ENGINE **NO 5D16611281** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **BGA//RB/1137/2020**

115849802

### KUPOTEA KWA KADI

**Sarita Octavian Mageni** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T507 DEJ** aina ya **IST-TOYOTA.** Kadi hiyo imetolewa na mamlaka ya mapato. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/MAG/RB/585540/2020**

115848702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi 123 2020**

**Ombi la SAFILA NOTTI DIMA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu RAJABU MAKAME ERNEST**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 7/9/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tareha 6/8/2020

115848602

### KUPOTEA KWA KADI

**Karim Shabani Leveri** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T186 BEA** aina ya **SUZUKI CARRY.** Kadi hiyo imetolewa na mamlaka ya mapato. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/SEL/RB/553693/2020**

115849302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA ARDHI NAMBA 35 YA MWAKA 2016**

**HABIB MSAFIRI NKAMIA...............................MDAI**
**DHIDI YA**
**ACCESS BANK TANZANIA LTD.................1. MDAIWA**
**MBOGO AUCTION MART & REAL AGENCY CO.LTD.........2.MDAIWA**
**AKIBAR YUSUF..........................................3. MDAIWA**

**KWA: MBOGO AUCTION MART & REAL AGENCY LTD, DAR ES SALAAM**
**AKIBAR YUSUF, DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kwa mdai alitajwa hapo juu ameefungua shauri la ardhi dhidi yenu shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya madai zinazopatikana katika Mahakama hii hivyo basi kama mmoja wa wadaiwa unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 10 Agosti, 2020 saa nne (10:00) kamili mbele **MHE.JAJI L. M. MLACHA** jujibu madai dhidi yenu. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika usikilizaji wa shauri hili.

**ANGALIA:**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikathibitisha kuwa umepokea wito huu basi shauri litasikilizwa na kutolewa maamuzi bila wewe mwenyewe kuwepo

**HATI** hii imetolewa kwa mkono wangu na CHAPA ya Mahakama leo hii tarehe 6 Mwezi 8 2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM

115848502

### KUPOTEA KWA KADI

**Bahati Selefiana Kakolelo** Mkazi wa Wilaya ya Busega Mkoani Simiyu anatangaza kupoteza kadi yake ya pikipiki aina na SANLG yenye namba za usajili **MC 227** BRH,Injini namba **17915607 na** cheses namba **lbrspjb54h901235** Kadi hiyo ilipotea julai 14 2020 wakati akihamisha mizigo yake kwenda kwenye nyumba nyingine. Anaomba yoyote atakayekuwa ameiokota aiwasilishe katika kituo cha polisi Wilayani Busega.
Taarifa imetolewa kwa Polisi
**Taarifa: SIM/BUS/RB/578173/2020**

115849402

### KUPOTEA KWA KADI

**NICODEMAS HENRY MAGANGA ANATANGAZA** KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SCANIA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 988 DLB / T 528 CPG** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
**KAH/ TR /RB/ 283 /2020.**

115849502


Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB:
+255 - 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# CAVANI SASA KUTUA BRAZIL



**PARIS,** Ufaransa

MAJALIWA ya Edinson Cavani sasa yanaonekana kuwa atarudi bara la Amerika Kusini kumalizia soka lake.

Kwa mujibu wa Globo Esporte, Cavani anaonekana kukaribia kujiunga na miamba wa Brazil, Atletico MG.

Nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay mkataba wake kule klabu ya PSG ya Ufaransa umemalizika mwishoni mwa msimu huu na hivyo anaondoka akiwa mchezaji huru.

Tayari alikuwa akihusishwa na klabu kadhaa, ikiwamo Inter Miami ya Merakani na Leeds United, mara tu baada ya kubainisha kwamba, anaondoka pale Paris Saint-Germain.

Ripoti zaidi zinasema kwamba, mfungaji huyo wa wakati wote wa PSG hana mpango wa kubakia barani Ulaya na kwamba ameamua kwenda kumalizia soka lake bara la Amerika Kusini.

Alikuwa pia akihusishwa na kuwaniwa na klabu ya Newcastle United ya Ligi Kuu ya England, kabla ya dili hilo kuyeyuka.




## Wolves yapania mafanikio Ulaya

**LONDON** England

MSHAMBULIAJI Raul Jimenez amesema Wolves inataka "kuwa na mafanikio makubwa" baada ya kutinga robo fainali ya Ligi ya Europa kwa kuifunga Olympiakos.

Penalti ya Jimenez iliiwezesha timu hiyo kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya mabingwa hao wa Ugiriki kwenye Uwanja wa Molineux, juzi Alhamisi na hivyo kuwa na ushindi wa uwiano wa mabao 2-1.

Hii ni mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 48 Wolves kutinga hatua hiyo katika mashindano hayo ya Ulaya.

"Tunataka kuendelea mbele. Tunaweza kufanya hivyo," alisema Jimenez.

Aliiambia BT Sport: "Ni muda mrefu. Tulianza kama mwaka na sasa tupo hapa. Ni jambo kubwa."

Wolves, ambao walianza msimu siku 383 zilizopita, watacheza na washindi mara tano wa mashindano hayo, Sevilla kwenye mchezo wa robo fainali mjini Duisburg, Jumanne ijayo.

## Roma yauzwa kwa bilionea wa Marekani

**ROME,** Italia

TAJIRI bilionea wa Marekani, Dan Friedkin amesaini mkataba wenye thamani ya euro milioni 591 kuinunua klabu ya AS Roma ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

"Tunaangalia kununua kila kitu kadiri itakavyowezekana na sisi kuwa sehemu ya familia ya AS Roma," alisema Friedkin katika taarifa yake.

Inatarajiwa kwamba dili hilo litakamilika mwishoni mwa Agosti mwaka huu na yeye kumilikishwa klabu hiyo.

Hii ni mara ya kwanza kwa bilionea Friedkin kuwekeza kwenye michezo, kwani uwekezaji wake mkubwa umekuwa kwenye magari na hospitali.

Ataichukua Roma kutoka kwa kampuni ya kibiashara ya Marekani inayoongozwa na James Pallotta, ambaye aliinunua klabu hiyo mwaka 2012.

Chini ya Pallotta, Roma ilimaliza kwenye msimamo wa Serie A kama washindi wa pili mara tatu na ikatinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2018 kwa kuiondoa Barcelona.



HABARI MICHEZO

# Inter Milan yathibitisha kumsajili Sanchez

**MILAN,** Italia

INTER Milan imethibitisha kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Alexis Sanchez kwa mkataba wa kudumu.

Sanchez amesaini mkataba wa miaka mitatu wa kuwachezea miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia katika kikosi hicho cha kocha, Antonio Conte.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 raia wa Chile, alijiunga na United akitokea Arsenal mwaka 2018, lakini alishindwa kuonyesha kiwango chake pale Old Trafford.

Sanchez ameripotiwa kwamba amejiunga na Inter akiwa mchezaji huru baada ya United kusitisha mkataba wake, ambao alikuwa akilipwa mshahara wa pauni 560,000 kwa wiki.

Amefunga mabao manne katika mechi 29 alizowachezea Nerazzurri tangu alipotua hapo San Siro, Agosti mwaka jana.

Sanchez alifunga mabao matano tu katika mechi 45 alizowachezea 'Mashetani Wekundu' tangu alipotua klabuni hapo Januari mwaka 2018 katika dili ambalo lilimhusisha Henrikh Mkhitaryan kwenda Arsenal.






# ZIDANE: BALE ALIKATAA KUIVAA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

GARETH Bale "hakutaka kucheza" kwenye mchezo wa pili wa mtoano wa timu 16-bora dhidi ya Manchester City, amesema kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane.

Mshambuliaji huyo wa Wales, Bale aliachwa katika kikosi cha Real cha wachezaji 24 kilichoivaa Man City jana Ijumaa.

Mchezaji hyo mwenye umri wa miaka 31, ameanza katika mechi 14 tu kwenye mashindano yote msimu huu wa 2019-20 na amecheza mara mbili tu tangu kurudi kwa Ligi Kuu Hispania Juni, mwaka huu.

"Yalikuwa majadiliano binafsi kati yangu na yeye. Aliamua kutocheza," alisema Zidane.

"Mengine yote yanabakia kati yangu mimi na yeye, lakini alisema hataki kucheza."

BBC Sport inaelewa kwamba, Bale aliamua kutosafiri na Manchester kwa sababu alijua hana nafasi ya kucheza kwenye mchezo huo.

City walishinda 2-1 kwenye mchezo wa kwanza uliopigwa nchini Hispania kabla ya mashindano hayo kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# *Garcia kakataa kusaini mkataba mpya - Guardiola*

**MANCHESTER,** England

ERIC Garcia anaonekana kuondoka Manchester City baada ya kumwambia Pep Guardiola hataki kusaini mkataba mpya.

Mlinzi huyo, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, amekuwa akihusishwa na uwezekano wa kuhamia Barcelona.

Akizungumzia kuelekea mchezo wa jana Ijumaa dhidi ya Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Guardiola alithibitisha Garcia amekataa nafasi ya kuongeza mkataba wake wa kukaa hapo Etihad.

"Alitutangazia sisi kwamba hataki kuongeza mkataba na Manchester City," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake. Tunamtaka, lakini hataki kuongeza mkataba mpya."

Garcia alijiimarisha yeye mwenyewe kwenye kikosi cha kwanza cha Man City akiwa patina wa Aymeric Laporte.

Garcia amecheza mechi 22 katika mashindano yote hapo Man City tangu alipojiunga nayo mwaka 2017.

Alihitimu katika akademi ya kukuza soka la vijana pale La Masia katika klabu ya Barcelona.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG KUSAINI MKATABA MPYA ARSENAL

## Kwa muda mrefu amekuwa akitajwa kuwaniwa Barcelona na Madrid, lakini sasa...

**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang anakaribia kumaliza uvumi kuhusu majaliwa yake kwa kusaini mkataba mpya pale Arsenal.

**Kumekuwa na uvumi wa muda mrefu kwamba, Aubameyang anataka kondoka Arsenal kipindi hiki cha majira ya joto, huku klabu kadhaa zikihusishwa kusaka saini yake.**

Kwa mara ya kwanza gazeti la Daily Telegraph, limeripoti kwamba, Aubameyang anakaribia kusaini mkataba mpya ambapo mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu ujao.

Aubameyang amefunga mabao 22 kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu na kufunga mawili wakati Arsenal ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Chelsea kwenye fainali ya Kombe la FA.

Tangu alipotua pale Arsenal akitokea Borussia Dortmund Januari mwaka 2018, amefunga mabao 54 katika mechi 85 za Ligi Kuu.

Aubameyang mwenye umri wa miaka 31, ni mdogo kwa Willian mwenye miaka 32, ambaye amepewa mkataba wa miaka mitatu baada ya kutoka kule Chelsea akiwa mchezaji huru.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon kwa muda mrefu amekuwa akitajwa kuwania na klabu za Barcelona na Real Madrid.

Baada ya fainali ya Kombe la FA, Aubameyang alibainisha kwamba, hajui hatima yake na hivyo hawezi kuzungumzia lolote.

"Kwa sasa nafurahia Kombe la FA, ni furaha tu, sijui kuhusu majaliwa yangu," alinukuliwa akisema.

Nyota huyo ambaye alitua Arsenal kwa kitita kikubwa zaidi cha fedha cha pauni milioni 50, amekuwa nguzo kubwa kwa kikosi hicho msimu huu na kukiwezesha kubeba taji la FA.

Imeripotiwa kwamba, mchezaji huyo alikuwa anataka mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki ili aweze kusaini mkataba huo mpya.

## ZISIKUPITE

### BARCA KUTWAA BEKI LEICESTER

BARCELONA inajiandaa kuwasilisha dau la pauni milioni 35.9 kwa beki wa Leicester City mwenye umri wa miaka 24 raia wa Uturuki, Caglar Soyuncu. ***(NTV Spor)***

### WILLIAN ASAINI 3 ARSENAL

WINGA wa Chelsea na Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 31, amekubali kutia saini mkataba wa miaka mitatu na klabu ya Arsenal ambapo atakuwa akilipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. ***(ESPN)***

### SILVA AWANIWA LAZIO

KLABU ya Lazio ina imani ya kukamilisha usajili wa kiungo wa kati wa Manchester City, David Silva. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, atakuwa huru mwisho mwa msimu huu. ***(Sky Sports)***

### UNITED KUMUUZA LENGARD

MANCHESTER United itasikiliza ofa za kumuuza kiungo wa kati raia wa England, Jesse Lengard mwenye umri wa miaka 27. ***(Guardian)***

### WEST HAM OFA YA RICE BADO

KLABU ya West Ham haijapokea ombi la kumuuza beki wa kati wa England mwenye umri wa miaka 21, Declan Rice kwa mujibu wa meneja wake. ***(Sky Sports)***

### SPURS YAMUWANIA WILSON

TOTENHAM Hotspur itaanza kumfuatilia mshambuliaji wa England na Bournemouth mwenye umri wa miaka 28, Callum Wilson. ***(Express)***

### EVERTON KUMSAJILI DALOT

KLABU ya Everton inalenga kumsajili mlinzi wa Manchester United na Ureno mwenye umri wa miaka 21, Diogo Dalot. ***(Star)***

### TERRY ATAJWA B'MOUTH

KOCHA msaidizi wa Aston Villa, John Terry ameorodheshwa katika nafasi ya kuchukua mikoba ya ukocha mkuu wa klabu ya Bournemouth. ***(Metro)***

### LEEDS YAMWANIA GONZALEZ

KLABU ya Leeds United inapanga kumsajili mshambuliaji wa Argentina na Stuttgart, Nicolas Gonzalez mwenye umri wa miaka 22, usajili utakaowagharimu pauni milioni 20. ***(Mirror)***

### UNITED YAMFUNGUKIA AKE

MANCHESTER United ndio ilikuwa klabu ya kwanza kutaka kumsajili mlinzi wa Uholanzi, Nathan Ake mwenye umri wa miaka 25, kabla ya kujiunga na Manchester City kutoka Bournemouth wiki hii. ***(Sky Sports)***

### LEEDS KWA BENRAHMA

KLABU ya Leeds imejiandaa kuwasilisha ofa ya kumsajili winga wa Brentford na Algeria, Said Benrahma mwenye umri wa miaka 24. ***(Telegraph)***



HABARI MICHEZO

## KMC, JKT Tanzania zamuwinda Kibaya

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Mtibwa Sugar, Jaffer Kibaya ameingia katika rada za kutakiwa na JKT Tanzania pamoja na KMC kwa ajili ya kuimarisha safu ya ushambuliaji ya timu hizo kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza jana Makamu Mwenyekiti wa JKT, Thabeet Barajah alisema wapo katika mazungumzo na mchezaji huyo ambaye amemaliza mkataba na timu yake ya Mtibwa na mambo yakiwa mazuri msimu huu atakuwa mali yao.

Alisema nyota huyo ni mapendekezo ya benchi la ufundi ambalo linahitaji kufanya maboresha kidogo ikiwamo nafasi ya ushambuliaji ambayo anatajwa Kibaya, huku pia wakihitaji kiungo mkabaji na beki wa kushoto wakimtupia jicho Zuberi Dabi wa Ruvu Shooting.

"Kibaya ni mchezaji mzuri na kocha amependekeza jina lake hilo suala hilo lipo kwa Mwenyekiti wetu, Hassan Mabena kwa ajili ya kumalizana na nyota huyo ili kupata huduma yake," alisema Barajah.

Alisema msimu huu watafanya usajili mdogo kutokana na kocha kuridhishwa na viwango vya wachezaji walioitumikia klabu hiyo msimu uliomalizika.

Naye Kibaya alithibitisha kufanya mazungumzo na JKT Tanzania akisema: "Nimemaliza mkataba na Mtibwa Sugar, JKT naendelea kufanya mazungumzo nao, lakini mbali na mabosi wangu hao wa zamani, pia KMC FC nao wanahitaji huduma yangu naendelea kuwasikiliza," alisema Kibaya.

## ZFF yamfungia refa kuchelewa uwanjani

**Na Hawa Abdalla,** ZANZIBAR

KAMATI ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) limemsimamisha mwamuzi wa kati Juma Makame Vuai kutochezesha mechi zote zilizosalia katika msimu huu wa 2019/2020 kwa kitendo cha kuchelewa kufika uwanjani kutekeleza majukumu yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati hiyo, Muhusini Kamara, alisema mwamuzi huyo alichelewa kufika uwanjani kuchezesha mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kati ya Black Sailor na Kikwajuni katika Uwanja wa Mau uliopangwa kuanza juzi saa 8:00 mchana, hivyo mechi hiyo kuchezeshwa na mwamuzi wa akiba.

Alisema mwamuzi huyo alifika uwanjani robo saa baada ya mchezo kuanza kitendo ambacho ni kinyume cha kanuni za mpira wa miguu duniani.

"Kitendo alichokifanya hakikubaliki katika soka na ni kosa kubwa kwa mwamuzi kushindwa kuzingatia muda wakati alikuwa anajua mchezo huo utachezwa muda gani, huku akiwa yeye ni mwamuzi wa kati," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa Kamati ya Waamuzi itaendelea kuhakikisha waamuzi wote wanazingatia nidhamu katika majukumu yao hususan suala la muda pale wanapopangiwa wajukumu yao.

# AZAM BADO WANNE TU, SHIBOUB ATAJWA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam imesema imebakisha wachezaji wanne tu ili wafunge usajili wa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, huku wakihusishwa kufikia hatua nzuri ya kumsajili kiungo wa Simba, Msudan Sharaf Eldin Shiboub.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia, alisema kuwa baada ya kufanya usajili wa wachezaji wanne kwa matakwa ya kocha wao mkuu, Aristica Cioaba, bado inatarajia kufanya usajili wa wachezaji wengine wanne, wawili wakiwa ni kutoka nje ya nchi.

Tayari Azam imemsajili Awesu Awesu kutoka Kagera Sugar, Ally Niyonzima kutoka Rwanda, Ayoub Lyanga wa Coastal Union, Ismail Aziz kutoka Prisons na Kipa David Kissu aliyemaliza mkataba na Gor Mahia ya Kenya.

**"Tayari, tumesajili kiungo mshambuliaji Awesu, kiungo wa kukaba Niyonzima, winga Lyanga, winga Ismail, na kipa Kisu, sasa tumebakisha nafasi nne tu kumalize rasmi usajili msimu huu, hivyo bado tutaendelea kutangaza kadri tutakavyokuwa tunasajili," alisema Zacharia.**

Alisema baada ya usajili huo, wamebakisha usajili wa wachezaji wawili tu wa kigeni, na wawili wazawa.

"Nafasi ambazo zimebaki kwa mujibu wa kocha wetu ni beki wa kulia na kushoto, kiungo mmoja mshambuliaji na mshambuliaji, hapo tutakuwa tumefunga usajili kwa wachezaji tisa waliokuwa wanahitajika," alifafanua.

Ingawa hakutaja majina ya wachezaji hao, lakini taarifa zilizolifikia Nipashe kutoka chanzo chetu ndani ya Azam, zimeeleza kuwa kuna mazungumzo yanaendelea kati ya klabu hiyo na Shiboub, ambaye anaelezwa kumaliza mkataba wa kuitumikia Simba.

Kiungo huyo mrefu, anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, kwa muda mrefu amekuwa hana namba kwenye kikosi cha kwanza cha Simba na klabu yake imeonekana kuwa haina nia ya kumwongeza mkataba mwingine baada ya ule wa awali kumalizika.

KONDE...




Bondia Salum Mohamed (kulia) wa Jeshi la Magereza, akimrushia konde Dani Leonard wa JKT katika Mashindano ya Taifa ya wazi yanayofanyika katika viwanja vya Tanganyika Peckers jijini Dar es Salaam. Katika shindano hilo lililofanyika Jumanne wiki hii, Mohamed alishinda kwa pointi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mnyate aachwa Ruvu Shooting ikitema wa5*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ruvu Shooting ya mkoani Pwani, imeacha wachezaji watano ambao haitakuwa nao kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Masau Bwire, amesema wachezaji hao wameachwa baada ya ushauri wa benchi la ufundi chini ya Kocha Mkuu, Salum Mayanga.

Akitangaza wachezaji hao, Masau aliwataja kuwa ni Rajab Zahir, mchezaji wa zamani Yanga, Jamal Mnyate, mchezaji wa zamani wa klabu za Simba, Azam na Mwadui pamoja na mchezaji wa zamani wa Simba na Kagera Sugar, Edward Christopha. Wengine ni Salum Makota na Adam Faraja.

Alisema baada ya hapo kinachofuata ni utekelezaji wa kuboresha kikosi kwa ajili ya msimu ujao wa ligi. Bwire alisema kinachofuata sasa ni viongozi kutangaza wachezaji watakaowasajili, na siku si nyingi wataanza kufanya hivyo.

"Baada ya kupata ripoti kutoka kwa kocha Mayanga, tumetangaza kuwaacha wachezaji hao ambao kwa sasa wapo huru kujiunga na klabu yoyote ile, kwa hiyo sasa kinachofuata ni usajili na tutasajili kwa kufuata maelekezo ya mwalimu kwa sababu yeye ndiye anajua kikosi chake kilikuwaje, kibadilike vipi na nani asajiliwe, nani atoke," alisema msemaji huyo.

Kuhusu wachezaji wao kutakiwa na klabu zingine, Bwire alisema kama wapo wao hawana pingamizi kwa sababu wanatafuta maisha, lakini aliongeza kuwa kwa jinsi Ruvu Shooting ilivyo na inavyojali wachezaji, hadhani kama kuna mchezaji anatamani kutoka.

Michezo
Jumamosi Agosti 8, 2020
Nipashe



Aubameyang kusaini mkataba Arsenal

UKURASA 22

ATATANGAZWA?...



Kiungo wa Yanga, Bernard Morrison, anayehusishwa kumwaga wino Simba. **PICHA: MTANDAO**

## Sven kuongezwa mwaka Msimbazi

**Na Saada Akida**

HATIMAYE Bodi ya Wakurugezi ya Simba imekubaliana kwa pamoja kumwongeza mkataba mpya Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck kwa ajili ya kuendelea kukinoa kikosi cha timu hiyo baada ya kuridhishwa na mafanikio aliyowapa msimu huu.

Hivi karibuni kulikuwa na sintofahamu juu ya Sven kubaki au kutafutwa mbadala wake hali ambayo iliwaumiza vichwa viongozi hao na sasa hatima ya Mbelgiji huyo ni kuongezewa mkataba wa mwaka mmoja wa kukinoa kikosi cha timu hiyo kwa mara nyingi.

Taarifa za uhakika kutoka ndani ya klabu hiyo zilizolifikia gazeti hili ni kwamba, baada ya kupitia ripoti waliokabidhiwa uongozi umechukuwa jukumu la kuhakikisha unamrejesha kocha huyo kwa kumwongezea mkataba ili kwenda sambamba na mipango yao ya msimu ujao.

Mtoa habari huyo alisema maamuzi hayo yametoka baada ya wajumbe wa bodi hiyo kutafakari kwa kina pamoja na kuangalia mahitaji yao ya kutetea ubingwa wao pamoja na kuwafikisha mbali kuvuka hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kuna mambo mengi ambayo yamezingatiwa kabla ya kuchukua uamuzi wa kumwondoa kocha huyo, ukiangalia muda uliobaki ni mdogo sana, suala la kuleta mbadala wake pia wachezaji waje kufuata mfumo wake itachukuwa muda mrefu ilhali Sven ataendelea pale alipoishia," alisema mtoa habari huyo.

Alisema uongozi haukuona sababu ya kumwondoa haraka kocha huyo ambaye yupo kwao Ubelgiji akisikilizia hatima yake, na kwamba wanaimani ataweza kufikia malengo yao kutokana na tayari wachezaji waliokuwapo wanaufahamu vizuri mfumo wa kocha huyo.

# Morrison, Simba kimyaaa

### ●●● Ndivyo kama mlivyosikia, tajiri Yanga asema subirini muone, aanika mazito huku akishangaa...

**Na Mwandishi Wetu**

FUKUTO la usajili Ligi Kuu Bara linazidi kupanda huku kiungo mshambuliaji wa Yanga, Bernard Morrison na mabingwa wa ligi hiyo nchini, Simba wakizidi kupiga kimya kizito baada ya pande hizo mbili kuhusishwa kuingia mkataba wa kufanya kazi pamoja kuelekea msimu ujao.

**Kwa muda mrefu Morrison amekuwa katika mvutano na klabu yake ya Yanga baada ya kumaliza mkataba wa awali wa miezi sita na kudaiwa kusaini mwingine wa miaka miwili wa kuendelea kuitumikia miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, jambo ambalo analipinga.**

Morrison amekuwa akidai kwa nyakati tofauti kuwa, hajasaini mkataba mpya na huo unaoelezwa saini yake imeghushiwa, ambapo suala hilo kwa sasa lipo Shirikisho la Soka nchini (TFF), likisubiri kuamuliwa.

Hata hivyo, jana habari zilizagaa jijini Dar es Salaam zikidai kuwa tayari Morrison ameshasaini mkataba na Simba na anatarajiwa kutangazwa muda wowote kuwa mchezaji halali wa timu hiyo.

Na alipotafutwa Mkurugenzi wa Uwekezaji ndani ya GSM ambao ni wadhamini wa Yanga, Injinia Hersi Said kuzungumzia suala hilo, alisema atashangaa kama Simba itafanya hivyo wakati bado Morrison na Yanga wana kesi katika Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF.

Alisema anaamini Simba ni weledi wa kufuata taratibu na haiwezi kufanya hivyo, na kwamba haraka haraka amenza kuona kuna jambo ambalo limemfanya Morrison kuwa na jeuri kiasi hicho.

"Tulikuwa tunashangaa anapata wapi jeuri kwetu ya kuonyesha utovu wa nidhamu kiasi hicho, wakati sisi ndio tumemleta nchini, kwa hiyo wao ndio walikuwa wanampa jeuri, lakini naiheshimu sana Simba kwa kuendesha mambo yao kwa kufuata taratibu, hivyo nitashangaa kama atatangazwa [kusajiliwa Simba]," alisema Injinia Hersi.

Alisema akiangalia anaona picha mbaya kama mchezaji huyo atasaini huku akifafanua kuwa Morrison amekuwa akisema kwamba viongozi wa Simba wamekuwa wakimlaghai ili kumpa mkataba hivyo kama atatangazwa basi itatoa picha kwamba Wekundu wa Msimbazi hao walikuwa nyuma katika suala hilo.

Wakati Yanga ikiendelea kujifikirisha kuhusu suala hilo, Morrison jana alikuwa hana hili wala lile, zaidi ya kuendelea kufanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam akiwa na Team Kiba inayotarajiwa kumenyana na Team Samatta, mechi hiyo ikihusisha mastaa mbalimbali kutoka Simba na Yanga.

Kwa upande wa Simba hakuna kiongozi yeyote aliyekuwa tayari kuzungumzia suala hilo, zaidi ya kueleza wachezaji watakaosajili watawatangaza hivi karibuni.

Lakini chanzo chetu ndani ya Simba kililiambia gazeti hili: "Morrison atatua Simba, labda tuamue kuachana naye, tayari kila kitu tumechungulia na kubaini hana mkataba na Yanga."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >